

Maagizo Ya Gabrieli Kwa Danieli

 Bwana akubariki, ndugu. Habari za asubuhi, wapendwa. Ni joto sana, kuwa katika maskani asubuhi ya leo, lakini ni jambo la fahari sana kuwa hapa. Nina furaha sana ya kwamba tungeweza—tungeweza kuingia leo kwa ajili ya ibada hii. Na imetangazwa ya kwamba ningekuwa na somo sasa juu ya haya *Majuma Sabini ya Danieli*. Hizo zinaunganisha ile sehemu nyingine ya Ujumbe kabla sijaendelea na ile—ile Mihuri Saba. Ambapo ni, Mihuri Saba; Mapigo saba; Baragumu Saba; Ole Tatu; yule mwanamke katika jua; kutupwa nje kwa Pepo yule Mwekundu; wale mia na arobaini na nne elfu walioitiwa muhuri; yote yanatukia katikati ya wakati huu. Nami nilifikiri itanibidi ningize hili kwanza.

² Sasa, kuna joto. Hatukusudii kukaa sana, kama tu tuwezavyo. Na huu ndio msimu, kwa kawaida, msimu wa likizo, ambapo watu hawaendi kanisani mara nyingi. Na, zaidi sana, na wote wana vyumba vyenye vibaridishi, na kadhalika, ambamo ni starehe. Laiti tungalikuwa na hayo, lakini kwa wakati huu hatuna.

³ Wengi wa babu zetu waliketi kwenye juu kali. Ninapofikiria juu ya kuomba msamaha kwa watu kwa kutokuwa na chumba chenye kibaridishi, mawazo yangu daima hupeperushwa mpaka Afrika ambapo walikaa kule kwenye zile tufani, na hao wanawake na nywele zao zikining'inia usoni, walikaa hapo mchana na usiku pia, bila kuondoka hata kidogo mahali walipokaa; hawali, hawanywi, wala cho chote kile, walikaa papo hapo tu ili wapate kusikia Neno moja, ama mawili, ya Bwana, mara kwa mara.

⁴ Ninaweza kukumbuka Mexico wakati ilikuwa kuna joto sana hatia, kwa kweli, niliketi kwenye chumba cha kondishani na nikajaribu kujipepea, kulikuwa na joto sana. Na unawaona hao watu wakiwasili pale kwenye saa tisa za usiku, kwenye uwanja ule mkubwa wa michezo, na hawana viti, vya kuketi chini. Wagonjwa, wagonjwa hasa, wanaokufa, wagonjwa; kansa, kivimbe; na mama wagonjwa, watoto wachanga, wanaokufa na kadhalika, wamesimama papo hapo kwenye hilo juu kali linalochemka, bila kivuli mahali po pote, na mmoja akimwegemea mwингine tu tangu saa tisa za usiku mpaka saa tatu za usiku wa pili, ili wasikilize tu kwa dakika thelathini kupitia kwa mkalimanii, na kuona kazi za Bwana. Wanaketi pale na kungojea, wamevaa nguo kubwa nzito zilizochakaa, wanazivaa hizo majira ya baridi na kiangazi. Ndizo tu walizo nazo.

⁵ Na halafu ninafikiria juu ya kukaa kule kwenye misitu hiyo, jinsi ambavyo wangewaleta hao watu wagonjwa, ambaao

wasingeweza hata kusogea. Na huko India, wakati wao wangemlundika mmoja chini, halafu mwingine juu ya huyo, mwingine juu ya huyo, namna hiyo, wenye ukoma na magonjwa; ambapo wangewapitisha pole pole, na moja kwa moja huko barabarani, na kuwaweka kwenye hilo jua kali, linalochemka, jua la tropiki. Kwenye zile tufani, na umeme ukimulika, na mambo ya namna hiyo, wao wangelala papo hapo kwenye jua hilo na tufani, na kila kitu, bila kusogea wala kulalamika hata kidogo, ili kuninii tu...na kujaribu kupata Neno la Mungu, mara kwa mara, kitu fulani kwa ajili ya nafsi zao. Sasa kwa nini sisi tuombe msamaha asubuhi hii, tukiwa tuna dari juu yetu, feni zinazunguka? Tunapaswa kuona aibu kama tukilalamika juu ya jambo hilo.

⁶ Kwa hiyo ninakumbuka si muda mrefu uliopita, katika kisiwa fulani, kimoja cha visiwa huko katika Bahari za Kusini, nilikuwa na ibada kule usiku huo. Ndipo, loo, ikatokea tufani. Loo, sijapata kuona tufani kama hiyo, ni kimulimuli kimoja cha umeme baada ya kingine, vikiimulika hiyo nchi. Na jinsi upепо unavyovuma mpaka miti ilikuwa inalala kabisa chini. Nikasema, “Vema, wao ni ninii... Afadhalii nivue suti yangu, kwa sababu hakutakuweko na mtu ye yote kule.”

⁷ Punde lile gari dogo likarudi nyuma hata mlangoni, na mtu fulani akagonga mlango, tayari kuondoka.

Na nikamwambia kijana huyo, ye ye aliweza kuzungumza Kiingereza, nikasema, “Kuna mtu ye yote huko chini?”

Kasema, “Hata huwezi kufikia urefu wa jengo la mji kufikia mahali pale,” kwenye uwanja mkubwa wa mpira.

Ndipo nikasema, “Unataka kusema ya kwamba hao watu wako—wako huko nje namna hiyo,” nikasema, “tufani yote hii?”

Wakasema, “Wao wanataka kusikia habari za Mungu.”

⁸ Na—na kwa hiyo nikashuka nikaenda kule. Na kulikuweko na akina mama, vijana wasichana, matineja, si wakichekelea kipumbavu na kucheka, na kupasua futuza za peremende, wakizungumza mambo ya wavulana wao. Kila Neno, walilishikilia; wala hawakusogea, waliketi tu na kusikiliza. Nikafanya wito wa madhabahuni, kufanya tu wito wa madhabahuni, na maelfu wakasimama, huku majonzi yakiwatiririka machoni mwao namna hiyo, wamemwinulia Mungu mikono yao, wakiomba rehema kwa ajili ya nafsi yao, vijana wasichana na wavulana, umri wa miaka kumi na saba, kumi na minane. Siku hizi hata kwa namna fulani ni vigumu kuwafanya watu wazima wasikilize, mnaona. Hiyo—hiyo inaonyesha ya kwamba hatuna jambo la kunung’unikia. Mungu na ashukuriwe! Naam, bwana.

⁹ Tunetaka mambo yawe yote ya kisasa kama Wamarekani wengine, lakini hatuna ya jinsi hiyo; kwa hiyo tutaridhika tu na tulioyo nayo.

¹⁰ Sasa, nina jambo dogo nililoona ambalo ningetaka kulifanya hapa maskanini tena. Ni wangapi wana Biblia, inua mkono wako. Hebu na tufungue Zaburi ya 99 kabla hatujaomba. Tulikuwa tukifanya hivi, Ndugu Neville, miaka mingi iliyopita. Sijui kama... Je! mlikwisha kusoma Zaburi asubuhi hii? [Ndugu Neville anasema, "La."—Mh.] La. Ningetaka kuninii tu, kusanyiko, kusoma Zaburi.

¹¹ Leo asubuhi, nilipokuwa nimeketi kwenye chumba changu cha kusomea, nikiutafakari Ujumbe huu na Neno, nilifikiri "Mnajua, litakuwa ni jambo zuri tena ku—kuwafanya wote wasome Zaburi. Ninapenda kufanya hivyo sana."

Sababu ya mimi kuchelewa kidogo, walnipigia simu ya kutoka mbali, kutoka huko Cheyenne, kwa hiyo hiyo ndiyo sababu nilichelewa.

¹² Na sasa, wakati tunapofungua kwenye Zaburi hii, nina matangazo machache ninayotaka kutangaza, niliyopewa sasa hivi. Hiyo ni Zaburi ya 99.

¹³ "Tangu sasa, matangazo yote kuhusu mikutano hapa maskanini, na katika mikutano ya nje, yatatoka kwenye ofisi ya Jeffersonville. Mtu ye yote anayetaka kujua juu ya mikutano hana budi kujiandikisha, ama kuacha jina lake na anwani, na kuliweka mimbarani mwisho wa ibada usiku wa leo. Utatumia kijikaratasi cha taarifa mapema upate kujitayarisha kuhudhuria mikutano."

Hiyo ni kusema, kama mtu ye yote katika siku zijazo akitaka kujua ni wapi hasa tutakakofanya mikutano, tumeanzisha mfumo mpya, kwenye ofisi kule nje sasa, hivi kwamba unaweza tu kuweka jina lako na anwani hapa. Nasi tutakutumia kadi, mapema, ili ujue mahali mikutano hiyo inapoendelea, na labda na masomo yanayohusika, na cho chote kile kilichopo, kama ungeweza kupata nafasi. Unaona, kama huna mahali rasmi inapotokea, mtu mmoja anasema jambo *hivi* na mwininge anasema *vile*, hu—hulipati, unaona. Kwa hiyo hebu tu... Andika jina lako na anwani na kuliweka hapa, na Billy Paul atalichukua na kumpa mhusika.

¹⁴ Sasa, ililizwa, pia, kama kutakuweko na ninii zaidi... "Ndugu Branham, utakuwa na ibada nydingine zo zote za uponyaji maskanini, pamoja na upambanuzi?" La. La. Upambunuzi utatolewa na—na bodi yetu nydingine. Tuna Ndugu Neville hapa sasa ambaye ana kipawa cha unabii, ambaye anatabiria wagonjwa na kuwajulisha mambo wanayohitaji kujua. Na tuna ndugu mmoja jina lake Higg... Higginbotham, mmoja wa... alikuwa mdhamini, ametumika vizuri kwenye bodi. Simwoni asubuhi ya leo, lakini kwa kawaida yeye ana karama ya kunena kwa lugha. Na bibi mmoja mdogo jina lake Arganbright, dada mpendwa aliye na karama ya kufasiri lugha.

¹⁵ Na jumbe hizi zinathibitisha kwamba zinatoka kwa Mungu, kwa maana kwa kweli hazitolewi nje ya utaratibu, ziko katika utaratibu kabisa. Na mara karama hizi zitakapoanza kuongezeka, tutajaribu kuninii—kupata ninii...kuziweka sawasawa katika kanisa, jinsi ya kuzitumia. Nami nitaonana nao hivi karibuni sana, na ili kwamba ninii—ninii—mikutano hiyo itaendelezwa kikamilifu kabisa katika utaratibu wa Bwana, kikamilifu tuwezavyo kuiweka.

¹⁶ Lakini watu hawa wapendwa, ndivyo asemavyo jirani yangu, Bibi. Woods, ambaye amechomeka maikrofoni yake hapa, na kinasasauti kule nyuma, apate kuurekodi mikutano, kusudi tu apate jumbe hizo, na kuziorodhesha, na kuona kama ni za kweli ama ni za uongo. Mnaona? Hivyo ndivyo anavyozichunguza. Namjua Bibi. Woods kuwa ni mwanamke mwaminifu. Naye ananiambia juu ya mambo mengi ambayo yamesemwa, yanakuja kutimia.

¹⁷ Sasa, kwa hiyo tunashukuru kwa ajili ya jambo hilo. Ni msaada mkubwa jinsi gani jambo hilo lilitivo kwangu pale nyumbani, ninaporudi nyumbani, wakati huo. Huo upambanuzi upande wa kinabii hunichosha sana, na, kwa hiyo, Mungu amenitumia msaada kwa jambo hilo, kupitia unabii, na kunena kwa lugha, na kufasiri, ambako ni unabii. Ambako, ni unabii, kunena kwa lugha. Kuna watu wawili mbalimbali wanaotabiri. Mmoja ananena, mwingine akifahamu yale huyo mwingine anayosema katika lugha zisizojulikana, ni unabii hasa. Na sasa tutakuwa tukininii... Tuna jambo hilo kila siku, kila mikutano hapa wakati tunapokuwa na mistari yetu ya maombi katika mikutano.

¹⁸ Sasa, kuna mtu fulani basi angeuliza, ninii...juu ya karama. Ndiyo, ningali ninayo. Lakini kwa njia hiyo, namna pekee ninavyoitumia, ni katika mazungumzo ya faragha, ambayo huwa nayaafanya. Na, ili kuyapata, ninaamini wameyaandika hayo kwenye ubao wa matangazo kule nyuma, kupata ruhusa na kuweka wakati wako katika utaratibu, na Billy Paul, kijana wangu, kwa maana hapa ama kwenye mikutano baada ya hapa. Huko kazini, po pote pale, huna budi kuwa na kadi ndogo ambayo Billy Paulo atakupa. Kama kuna jambo fulani maishani ambalo huwezi kulielewa, wala hujui jinsi ya kuondokana nalo, nawe unatafuta hekima ya Bwana, basi hebu... Mwone Billy Paul, mwanangu, ambaye ndiye katibu, naye atakupa kadi ndogo, na kukupangia tarehe, kwa zamu.

Ndipo basi wakati tunapokuwa na mazungumzo hayo, basi wakati huo utakuwa ndio tutakapoingia ndani pamoja, wewe na mimi tu. Na endapo ni wanawake wanaokuja, utaingia na mimi pamoja na mke wangu. Ndipo utaninii... Tutapata kujua, na kumsihi Bwana na kumwomba yakulazimu ufanye nini.

¹⁹ Sasa, vingine, mambo madogo na kadhalika namna hiyo, yanapelekewa Ndugu Neville, na Ndugu Higginbotham, na Dada

Arganbright, na hao wengine wanaonena kwa lugha na kufasiri, ambao wako humu kanisani.

²⁰ Kwa hiyo, tuko kama katika safari. Ninaamini ilikuwa ni Yethro, aliyemwambia Musa siku moja, unaona, “Hebu na tuchukue baadhi ya wazee.” “Ndipo Roho wa Mungu akatolewa toka kwa Musa na kuwekwa juu ya wale wazee sabini, nao wakatabiri. Lakini ni mambo tu yaliyo muhimu na magumu ndiyo aliyopelekewa Musa peke yake.” Sasa, sisi si Musa, wala hawa si wale wazee, lakini tungali tunamtumikia Yehova Mungu, na Nguzo ile ile ya Moto ikiongoza kwenye Nchi ya ahadi.

Kwa hiyo, basi, naam, kutakuweko na wengine, kutakuweko na mikutano na kutakuweko na kufasi-... Upambanuzi utakuja. Jambo hilo litakuwa likinipa nafasi basi kuwa katika maombi na kusoma, siku ambazo ninajua ya kwamba mazungumzo haya yatakuja, nipate kuwa tayari kwa ajili yake.

²¹ Sasa kumbukeni, Billy Paul Branham, katibu wetu wa mikutano, ataninii... Yako kwenye... Matangazo yako kwenye ule ubao kule nyuma, yamewekwa na wadhamini. Nina muhtasari hapa wa kutangaza hayo, na kuwaambia watu wanaweza kuyasoma kwenye ubao wa matangazo, wakitoka.

²² Sasa, sasa, asubuhi ya leo tuna somo kubwa, na usiku wa leo tutajaribu kuendelea nalo. Na, Bwana akipenda, Jumapili ijayo, lingine, tutaendelea nalo. Sikujuu jinsi lilivyokuwa likiingia katika kilindi mpaka nilipoanza kulisoma. Na lingali ni siri kwangu, bado, na kwa hiyo ninamtegemea tu Bwana.

²³ Sasa, ninyi mlio na Biblia zenu, hebu na tufungue Zaburi 99, 99. Nami nitasoma aya ya 1, kusanyiko litasoma aya ya 2, kisha sote pamoja tutasoma aya ya mwisho. Tutaendelea mbele; mimi, ya 1; kusanyiko, ya 2; mimi, ya 3; kusanyiko, ya 4; na kuendelea hata aya ya mwisho, kisha sote tutaisoma pamoja.

Tafadhalii na tusimame tunapolisoma Neno la Mungu. [Ndugu Branham na kusanyiko wanasoma Zaburi ya 99:1-9 kama alivyoeleza—Mh.]

BWANA ametamalaki, mataifa wanatetemeka; ameketi katikati ya makerubi, nchi na inatikisike.

BWANA katika Sayuni ni mkuu, naye ametukuka juu ya mataifa yote.

Na walisifu jina lako kuu la kuhofiya; maana ni takatifu.

Nguvu za mfalme nazo zapenda hukumu; wewe ndiwe uliyeithibitisha adili; ulifanya hukumu na haki katika Yakobo.

Mtukuzeni BWANA, Mungu wetu; sujuduni penye kitu cha miguu yake; ndiye mtakatifu.

*Musa na Haruni mionganoni mwa makuhani wake,
na Samwel mionganoni mwao waliitiao jina lake,
walipomwita Bwana aliwaitikia;*

*Katika nguzo ya wingu alikuwa akisema nao.
Walishika shuhuda zake na amri aliyowapa.*

*Ee BWANA, Mungu wetu, ndiwe uliyewajibu; ulikuwa
kwo Mungu mwenye kusamehe ingawa uliwapatiliza
matendo yao.*

*Mtukuzeni BWANA, Mungu wetu; sujuduni
mkiukabili mlima wake mtakatifu; maana BWANA,
Mungu wetu, ndiye mtakatifu.*

- ²⁴ Na tuinamishe vichwa vyetu.

Hakika, Bwana, Maneno haya yameandikwa na kuchorwa na mtumishi Wako, Daudi, katika Zaburi Kwako. Wewe unaishi katikati ya Makerubi. Ndiwe mtakatifu, na kilima chako ni kitakatifu. Na tukaribie huku miyo yetu imenyunyiziwa Damu ya Bwana Yesu, tukiwa na dhamiri safi, na pamoja na imani na matumaini ya kwamba tunakuja katika Uwepo wa Mungu wetu. Jalia kusanyiko lote hili asubuhi ya leo liwe na uchaji. Fungua masikio yetu ya ufahamu. Nena kupitia kwetu, katika hekima, kusudi tupate kujuja jinsi tunavyoweza kuenenda katika siku hizi na katika Uwepo Wako.

- ²⁵ Tungekuomba Wewe, Mungu wetu, kutufunulia mambo haya ya siri ambazo zimefichwa miaka hii yote, tunapokaribia moja ya Maneno manyofu sana na yenye uchaji. Wewe ulinenia juu yake ulipokuwa hapa duniani, na kusema, "Yeye asomaye, na afahamu." Kwa hiyo, kwa neema kuu sana tunakuja Kwako, Bwana, na kutafuta hekima Yako, bila kujuja tu la kusema. Tumeponga hapa Maandiko machache, na kwa uchaji tukikutumainia Wewe kabisa tupate jibu, si kwa kusudi lingine bali kwamba tujue saa tunayoishi, tupate kuwa tayari kwa ajili ya mambo makuu yaliyo mbele. Tujalie jambo hilo, Bwana, katika Jina Lake Yeye aliyetufundisha sisi sote kwamba tunapaswa kuomba namna hii! [Ndugu Branham pamoja na kusanyiko wanaomba pamoja kulingana na Mathayo 6:9-13.—Mh.]

....Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe.

*Ufalme wako uje. Mapenzi Yako yatimizwe, hapa
duniani kama huko mbinguni.*

Utupe leo riziki yetu.

*Na utusamehe deni zetu, kama sisi nasi
tuwasamehevyo wadeni wetu.*

*Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu:
Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata
milele. Amina.*

²⁶ Ketini. Sasa, kama ye yote anataka kuvua koti lake, jisikie kufanya hivyo. Na wale wanaosimama ka—karibu na ukuta, kama miguu yenu ikiuma, mbona, jisikieni tu huru kutoka nje.

²⁷ Na sasa, nafikiri, kama watoto wanataka kwenda kwenye vyumba vyao, ama tayari wameenda? [Ndugu Neville anasema, "La, hawawezi. Hatuwezi kuwa nayo asubuhi ya leo, kwa sababu ya umati wa watu."—Mh.] Mchungaji anasema ya kwamba umati wa watu umejaa kwenye hivyo vyumba, kwa hiyo hatuwezi kuwa na shule ya Jumapili kwa watoto wadogo. Nasi tungefurahi kama ninyi watoto wadogo sasa mngeleshirikiana nasi, kwa kuwa asubuhi ya leo tutakuwa, tunaanza, Ujumbe muhimu sana, sana ambao nina hakika utakuwa na maana sana kwa baba yako na mama, na wapendwa wenu walio hapa, na hata kwenu ninyi watoto. Kwa hiyo, tunauendea kwa kicho sana.

²⁸ Bwana akipenda, asubuhi ya leo tunachukua somo la majuma sabini ya Danieli. Na asubuhi ya leo tutazungumzia juu ya Daniel akiwa uhamishoni, na Gabrieli akiruka kuja kumjulisha mambo yajayo. Wakati Danieli alipokuwa akiomba, Gabrieli, yule Malaika, alikuja kumjulisha.

Usiku wa leo, ninataka kuzungumza juu ya sababu sita za kuzuru Kwake, masomo sita mbalimbali yatakayoletwa usiku wa leo, aliyojia Gabrieli.

²⁹ Jumapili ijayo, Bwana akipenda, ninataka kuweka sababu na wakati wa zile Nyakati Saba za Kanisa, na kwamba ziko kwenye wakati gani, na mahali tunaposimama leo. Hiyo ni Jumapili ijayo asubuhi, Bwana akipenda.

³⁰ Sasa, sababu ya jambo hili. Nilikuja na mihitasari mifupi kutoka kwenye Jumbe zangu chache zilizopita. Na asubuhi ya leo ninataka kuyarudia kwa kifupi, kwa sababu huu unanaswa kwenye kanda za sumaku ambazo zitaenda ulimwenguni kote, mataifa mengi. Na, daima, sababu ya mimi kuyarudia kifupi, ni kwamba labda mtu fulani angesikia kanda hiyo kwa mara yao ya kwanza, na asingeweza kuelewa niliyokuwa ninamaanisha wakati ninaporejea nyuma kwenye jambo lingine.

³¹ Sasa tumechukua miezi mingi katika kujifunza Kitabu cha Ufunuo, Ufunuo wa Yesu Kristo. Tumepitia katika nyakati saba za kanisa. Sura tatu za kwanza za Ufunuo zilikuwa ni zile nyakati za kanisa. Halafu Yohana akatwalowi katika sura ya 4 na ya 5, na akaonyeshwa mambo ya—yatakayotokea baadaye. Sasa, kwenye sura ya 6, ye ye anashuka duniani tena, kuona mambo yakinukia ambayo yataendelea kutoka sura ya 6, aya ya 1, mpaka sura ya 19 na aya ya 21. Ndani hapa inakuja ile Mihuri, yale Mapigo, zile Ole, wale nzige, yu—yule mwanamke katika jua, na kutupwa nje kwa lile joka jekundu, kule kutiwa muhuri kwa wale mia na arobaini na nne elfu, na mambo haya yote.

³² Hili limekuwa ni juma la kusoma kwa ajabu sana. Jana, siku nzima, ilikuwa vigumu kwangu kuondoka chumbani, nikijaribu

kusoma. Na ni jambo fulani katika wakati wa mwisho, wengi wa watu wa zamani hapa, niliofundisha, nilisema tu, “Ndani humu kuna majuma sabini ya Danieli,” lakini sikujaribu kuyaingilia, kuyaelezea. Lakini wakati huu, kwa neema ya Mungu, nimechukua jukumu mimi mwenyewe kujaribu kuomba neema mbele za Mungu, ili kwamba niyalete kwa watu. Na ndani humu ninapata mambo ambayo sijui neno juu yake.

³³ Na, basi, ni-nimekuwa nikisoma kitabu cha Dk. Larkin, kitabu cha Dk. Smith, mihitasari ya Dk. Scofield, mafafanuzi mbalimbali ya watu kila mahali, na hata hivyo siwezi kuweka yao pamoja kuyafanya yawe sahihi. Mnaona? Kwa hiyo, juma hili ninapanga, nimekuwa nikitembelea maktaba huko Kentucky, juu ya baadhi ya elimu ya kale ya nyota kalenda na nyakati, na nikichukua kutoka kwenye maktaba mbali mbali, na kadhalika, vitabu vyote vya kale ninavyoweza, na yale madogo ninavyoweza kufanya, nami nikiweka matumaini yangu kwa uchaji katika Yesu Kristo kunifunulia.

Kwa sababu, sitaki iseme, “Ninajua jambo *hili*, na ninajua *lile*.” Yeye anajua moyo wangu. Ananisikiliza. Lakini ninazitaka, nipate kuwaangazia nuru watu Wake, kwa hiyo ninaamini ya kwamba Yeye atanipa hilo. Sijui bado, lakini ninamtumainia kwa ajili ya Jumapili ijayo, kwa maana hiyo ndiyo itakayokuwa sehemu iliyo muhimu sana, Jumapili ijayo, kuyajua na kuyaweka majuma hayo sabini.

³⁴ Kila moja lina mahali tofauti. Na unapofanya jambo hilo, ukiyapitia yote, hayaji sawa, hayaingii. Hayawezi. Na, kwa hiyo, na-naweza nisiyaweke sawa, lakini nitamtumainia Bwana kwa hilo.

³⁵ Nami ninakumbuka kuhusu Sulemani wakati mmoja akiomba na kumwuliza Bwana Mungu kama angempa hekima, si kwa ajili yake mwenyewe, “si kuongezewa siku, si maisha marefu, si utajiri,” lakini kwamba kwamba apate kuwa na hekima kujua jinsi ya—ya—ya kuwahukumu watu wa Mungu. Na Mungu akaliheshimu ombi hilo, na kumpa Sulemani hekima hiyo, kwa maana ilikuwa ni kwa ajili ya watu Wake. Na hiyo ndiyo sababu ninamwomba Mungu kuniruhusu njue haya majuma sabini yanamaanisha nini, kwa sababu ninajua ndiyo kalenda halisi kwa ajili ya wakati tunaoishi. Na, kwa hiyo, ninataka kujua jambo hilo; si kwa ajili yangu mwenyewe, mimi... si kwa ajili yangu mwenyewe. Maana, ninataka kujua. Sisemi hivyo, “Si kwa ajili yangu,” kwa maana ninataka jambo hilo kwa ajili yangu mwenyewe. Ninataka kujua, kwa sababu ninataka kujua mahali gani tunapoishi na ni wakati gani tunaoishi. Na, basi, ninajua ya kwamba amenipa hilo.

³⁶ Na watu mbalimbali wamekisia jambo hilo, nao wameliweka huko nyuma kabisa. Jamaa mmoja, nilikuwa nikisoma, aliyafanya yote kuishia katika mwaka wa 1919, yale majuma sabini. Vema, haikuwa hivyo.

Kwa hiyo, baada ya yale majuma sabini, baada ya yale majuma sabini, mambo yote yamekwisha. Kwa hiyo sisi—sisi hatuninii... Tunataka kujua Kweli. Nami ninamwomba Mungu anipe Kweli.

³⁷ Sasa, ili kuliwekea jambo hili msingi, kurudi nyuma, ninataka kurudia kidogo nyuma. Kwa hiyo, basi, mihitasari mifupi fulani niliyoandika, ambayo tulikuwa nayo katika sura ya 5, ya 4 na ya 5, ili kwamba watu wafahamu. Kwanza, kabla hatujafanya jambo hili, ninataka kurudia ya nyuma kidogo, ili kwamba mlipate kutoka ya 4...

Sasa, kumbukeni, sura ya 3 ilikuwa ni Wakati wa Kanisa la Laodikia, na Kanisa lilitwaliwa mwishoni mwa Laodikia.

³⁸ Sasa, nilikuwa nikijaribu kumwelezea mke wangu jambo fulani kuhusu hilo. Tulikuwa na Becky, binti yangu, pamoja na namna zote za kamusi mbalimbali na vitu ambavyo tungeweza kupata. Havinipi jawabu. Nikachukua kamusi ya Biblia. Nikachukua kamusi ya kale ya Kiyunani. Ni—ni kachukua Kamusi ya—ya Websters na nytingine nydingi, kamusi za kisasa. Hakuna hata moja ya hizo ingeweza hata... kutoa maneno ama jibu, kwa njia yo yote.

³⁹ Mke wangu akasema, “Unawatarajiaje watu wetu, amba ni watu maskini, na wengi wao hawana elimu kama sisi pia tusivyo nayo, kufahamu mambo kama hayo?”

Nikasema, “Mungu ndiye atakayetoea jibu.”

⁴⁰ Hata liwe gumu namna gani, Mungu anaweza kulivunjavanja na kulifanya rahisi. Kwa maana sisi ni... sehemu ya hao watu wanaotamani, wakiomba kwa ajili ya siku hiyo na saa hiyo. Na macho yetu yameelekezwa Mbinguni, nasi tunakungojea Kuja Kwake. Nami nina hakika tu ya kwamba Yeye atatuonyesha. Sasa, haitasema ni siku gani ama saa ipi, maana hakuna mtu atakayejua jambo hilo, lakini hakika itatwambia ile siku ya juma tunayoishi, kama tunaweza tu kuzifahamu.

⁴¹ Sasa, katika sura ya 4, Yohana alitwaliwa mara moja, baada ya Kanisa. Yohana, alipokwenda juu, aliona wakati mzima wa Kanisa. Hapo ndipo ningetaka kusimamia, kwa sekunde moja tu, kusema, ya kwamba: watu wengi wanaotarajia mambo fulani makuu, ya ajabu, jambo fulani lenye nguvu kutukia, katika wakati wa Mataifa, hakika wamekosea. Wakati wa Kanisa, na yote hayo yatakayotendeka katika utawala wa Mataifa, yameorodheshwa katika Ufunuo 1 hadi 3, yote pamoja. Halafu Kanisa lilinyakuliwa na kutwaliwa, na haya mengine, mpaka sura ya 19, ni yale yanayotendeka kwa taifa la Kiyahudi, baada ya Kanisa kwenda juu. Na ni wakati wa ile Dhiki kuu, hakuna kitakachotukia mionganini mwa Mataifa; ni mauaji tu, na kadhalika, kama tutakavyofikia jambo hilo na kuona.

⁴² Lakini Kanisa, Lenyewe, limeondoka kwenye ya 13... Kwenye aya ya mwisho ya sura ya 3 ya Ufunuo, wakati Wakati wa Laodikia utakapoisha, ambao ulikuwa ndio wa mwisho.

⁴³ Nasi tulichukua kila wakati wa kanisa, kila wakati, kila kitu kilichotukia, kila nyota, kila mjumbe, tabia yao, yale waliyofanya, na kulileta moja kwa moja katika historia mpaka yule wa mwisho kabisa, tukazichora pale pale kwenye picha, kwenye ukuta. Na wakati tulipomalizia, Roho Mtakatifu akaingia na kufanya duara ya jambo lile lile kwenye ukuta, na kulifunua Mwenyewe papa hapa kwetu sote.

⁴⁴ Sasa, katika kufanya jambo hili, ninatumaini, mwisho wa jambo hili Yeye atakuja na jambo fulani la ajabu sana na kutuonyesha sisi tena ya kwamba tuko kwenye wakati wa mwisho.

⁴⁵ Ni wangapi wenu walisikia ninii ya Kennedy... Hotuba ya Rais Kennedy, yale maoni na kadhalika? Ni wangapi walisikia ubashiri huu, ya kwamba ifikapo Januari 1, imebashiriwa ya kwamba Marekani na Urusi zote zitakuwa mavumbi ya volkeno? Hilo tu ndilo tunalohitaji. Wakati umeenda kuliko tunavyofikiria. Mnaona? Kwa hiyo, kama tumekaribia sana mpaka hata watu wa dunia hii wanabashiri jambo hili kubwa kutukia, afadhali tuwe macho, kila kitu kiwe sawa kabisa, toba zote zifanywe, kila kitu kiwe tayari, maana hatujui ni wakati gani Bwana wetu atakapotuita. Na wakati atakapotuita, "Njoni huku juu," afadhali uwe tayari. Na jambo hilo litatukia katika saa usiyowazia.

⁴⁶ Ule ufufuo mkuu wa Kipentekoste sasa unaisha. Tunauona kila mahali, ule hatua kuu ya mwisho. Ujumbe umetoka. Kila kitu kiko tayari sasa, kikingojea. Kanisa limetiwa muhuri. Walio waovu wanazidi kutenda maovu. Makanisa yanazidi kuwa baridi. Watakatifu wanamkaribia Mungu zaidi. Karama za Roho zinaanza kuongezeka katika yale makundi madogo. Tuko katika wakati wa mwisho. Loo, naupenda wimbo ule tuliokuwa tukiimba kanisani.

Ninatazamia kule kuja kwa ile Siku ya furaha
ya ule utawala wa miaka elfu,
Wakati Bwana wetu mbarikiwa atakapokuja
kumchukua Bibi-arusi Wake anayengoja;
Loo, moyo wangu unalia, ukiona kiu kwa ajili
ya siku hiyo ya kufunguliwa kutamu,
Wakati Mwokozi wetu atakaporudi duniani
tena.

⁴⁷ Tunangojea saa hiyo! Sasa, katika sura za 5 na aya ya 5, tunaona, katika somo letu lililopita, ya kwamba tulizungumzia juu ya yule Mkombozi aliye Jamaa ya Karibu, ambaye tuliona ya kwamba alikuwa ni Kristo. Alionyeshwa kwa mfano na Ruthu; Ruthu akiamua; Ruthu akitumika; Ruthu

akipumzika. Kuamua, kulikuwa ni kuhesabiwa haki; kutumika, akijitayarisha, kutakaswa; kupumzika, ilikuwa ni kuwa na Roho Mtakatifu, mpaka itakapokuja ile Karamu ya Arusi. Ni jambo zuri jinsi gani!

⁴⁸ Kanisa lilikuja kupitia kwa John Wesley, kuhesabiwa haki, ama... Martin Luther, kuhesabiwa haki; kupitia kwa John Wesley, kutakaswa; kupitia kwa Pentekoste, ubatizo wa Roho Mtakatifu; na sasa, linapumzika, likingojea Kuja kwa Bwana Wake. Barabara kabisa!

⁴⁹ Mkombozi wa Jamaa yetu, wale wazee walikuwa sahihi walipomwita Yeye Mwana-Kondoo, aliyekuwa karibu kuwa Simba, kama hakimu. Yeye alikuwa Mwana-Kondoo, mwajua, akiwa na kile Kitabu kilichotiya mihuri saba. Wakati Kitabu hicho kilipochukuliwa, kazi ya upatanisho ilikuwa imekwisha.

⁵⁰ Sasa, katika sura ya 3, Kanisa lilikuwa limenyakuliwa, lakini sasa ukombozi hauna budi kufunuliwa, jinsi Kanisa lilivyokombo—kombolewa, ufunuo wa yale yaliyotukia katika wakati wa Kanisa. Unaona, Kanisa limeondoka, kwa hiyo Yeye sasa anaonyesha, katika sura ya 5, jinsi vile alivyotimiza jambo hilo, yale yaliyotokea, jinsi alivyolitia Kanisa muhuri. Ufunuo wa Jina Lake; ubatizo wa maji, kwa kutumia Jina Lake; Uzima wa Milele; hakuna kuzimu ya Milele; uzao wa nyoka; usalama wa Milele; mafundisho yote muhimu, kuchaguliwa tangu zamani, kwa Kanisa, ambako kulifunuliwa kwa Kanisa. Yeye anaonyesha jinsi alivyofanya jambo hilo.

⁵¹ Sasa, Mtu wa Jamaa yetu anapewa Kitabu kilichotiya mihuri saba cha Ukombozi kutoka kwa Mwenyewe wa asili. Amina! Ni nani aliyekuwa, tunaona, alikuwa Mwenyewe wa asili? Mungu Mwenyewe. "Naye Mwana-Kondoo akaja akakitwaa kile Kitabu kutoka katika mkono wa kuume wa Yeye aliyeketi juu ya kile Kiti cha Enzi." Mwana-Kondoo alikuwa ni nani? Yule Mkombozi, Mkombozi aliye wa Jamaa yetu, wa Jamaa ya Kanisa, Ambaye alikuja akawakomboa Israeli.

⁵² Sasa tutaingilia jambo hilo asubuhi ya leo. Israeli walikombolewa, lakini huo haukuwahusu wao, maana walimkataa Yeye. Lakini, Kanisa lilipokea ukombozi wao, Naye ni Mkombozi wa Jamaa yetu. Kama vile Boazi alivyokuwa amemkomboa Naomi, kusudi ampare Ruthu, yule Mmoabu, mgeni, Mmataifa; vivyo hivyo Kristo aliwakomboa Israeli, akafanya ukombozi, na akakataliwa.

⁵³ Mnakumbuka ule msamaha, ambapo huyo mtu alipigwa risasi, ambao ninasimulia wakati mwingine? Katika vile vita vya wenyewe kwa wenyewe, wakati... Yeye alikuwa ni mtu mzuri. Hakuwa na hatia, nao wakampata na hatia. Ingawaje, alikuwa na hatia kwa namna fulani, kwamba alitoroka wakati wa vita. Nao wakampata na hatia na walikuwa wanataka kumpiga risasi. Ndipo mtu fulani akamwendea Raisi Lincoln

na kumwambia, "Bw. Lincoln, huyu mtu ni Mkristo. Aliogopa. Mvulana huyu, ninawajua ndugu zake. Alikuwa tu anaogopa. Hakutaka kufanya madhara yo yote. Alitoroka." Kasema, "Bw. Lincoln, liko mikononi mwako. Wewe ndiwe tu unayeweza kumsamehe."

Bw. Linoln akatwaa kipande cha karatasi na kalamu yake, na kutia sahihi, "Amesahehewa," huyu *Fulani*. "Abraham Lincoln."

Akarudi mbio gerezani, na kusema, "Hii hapa. Nimepata msamaha wako."

⁵⁴ Naye mtu huyo akasema, "Nakataa kuuangalia. Ungekuwa na muhuri mkubwa juu yake. Ungekuwa na kila kitu. Unajaribu tu kunifanya mpumbavu. Si Abraham Lincoln. Mtu ye yote angeweza kutia sahihi jina lake. Lakini ungepaswa kuidhinishwa kwa muhuri wake, na kadhalika, kama unatoka kwake." Na mtu huyo akamshawishi; ingawa mtu huyo aliyekuwa gerezani alifikiri ye ye aliakuwa anacheza, akaondoka tu akaenda zake.

Asubuhi yake, akapigwa risasi. Na basi baada ya kupigwa risasi, basi kulikuweko na kesi ya mahakama kuu, kwa sababu Abraham Lincoln, masaa ishirini na manne kabla mtu huyo hajapigwa risasi, alikuwa ametia sahihi jina lake ya kwamba mtu huyu amesamehewa. Na halafu serikali ikampiga risasi, hata hivyo. Vipi basi? Basi mahakama kuu ya Marekani, ikasema, ikafikia uamuzi huu kwa ajili ya mahakama Kuu, ikasema, "Msamaha si msamaha isipokuwa upokelewe kama msamaha."

⁵⁵ Naye Yesu aliwakomboa Israeli pale Kalvari. Lakini haukuwa ni msamaha kwao, kwa sababu hawakuupokea kama msamaha. Lakini, katika somo letu sasa juu ya majuma haya sabini, tunaona wao wanarudi na kupokea msamaha wao. Lakini, Yeye alilikomboa Kanisa, ndipo tunasamehewa kwa sababu tumepokea Damu ya Yesu Kristo kama msamaha wetu.

⁵⁶ Sasa, tunaona ya kwamba Yeye aliakuwa Mkombozi aliye wa Jamaa, Naye alikichukua kile Kitabu kutoka katika mkono wa Mwenyewe wa asili. Ni hati-miliki ya ukombozi. Tuliona jambo hilo. Mnakumbuka lile somo? Ni hati-miliki ya ukombozi. Ni hati ya siri inayoambatanishwa nayo, ya kwamba Mungu alihitaji uhai kwa mauti, katika bustani ya Edeni. Ndipo, Yesu, Yule mwenye haki, akafa na kuitwaa hiyo hati-miliki, naye akaweza kuvunja ile Mihuri, akafunua yale yaliyokuwa ndani Yake; na akatoa urithi, ambao ulikuwa ni mali Yake, kwa watu Wake. Uzima wa Milele, aliourithi kwa kufanya jambo hilo, Yeye aliurudisha Uzima Wake Mwenyewe, pale Kalvari, na kuugawanya kati yetu kwa Roho Mtakatifu. Amina! Hakuna mtu aliye pata (kamwe) kuja hata kuwazia juu ya upendo huo uliokuwako, yale aliye tunda Yeye!

⁵⁷ Shetani, aliyekuwa zamani ndiye yule anayemiliki kwa sababu ya lile anguko katika bustani, anafungwa na kutupwa katika Ziwa la Moto. Siku zake zimekwisha.

⁵⁸ Yesu, katika Injili, alikuwa na vyeo vinne. Tulipata jambo hilo. Mwana wa Daudi, mrithi kwenye Kiti cha Enzi; Mwana wa Ibrahim, cheo cha kifalme; Mwana wa adamu, mrithi wa dunia; Mwana wa Mungu, mrithi wa mambo yote. Cheo cha kifalme!

⁵⁹ Katika Agano la Kale, mali haingeninii—haingewekwa zaidi ya miaka hamsini. Haingaliondolewa kutoka kwa mwenyewe wa asili ila kwa miaka hamsini. Na katika siku ya arobaini Yeye alilipia gharama. Kwenye siku ya hamsini, ule ukombozi na zile nguvu zilizokuwa mali ya Kanisa, zilizopotea kwenye bustani ya Edeni, zilikombolewa na zikarudishwa, na kutumwa kwetu kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, katika siku ya hamsini.

⁶⁰ Ndipo tukachukua hili, lile gombo. Tulichukua yale magombo, jinsi ambavyo alikabidhiwa gombo hili mkononi Mwake. Jinsi ambavyo Yeremia, katika Yeremia 32:6, binamu Yake, Hanameli, alivyoachiwa urithi. Nao walikuwa wakienda uhamishoni. Ambako, tunaenda, pamoja naye, asubuhi ya leo, uhamishoni. Nayu iliwekwa katika chombo cha udongo; inaonyesha mahali ambapo nguvu za Mungu, na yale magombo pamoja na siri za Mungu, zinajulikana, moyoni. Mpango wetu wa ukombozi, nao vile vile umewekwa katika vyombo vya udongo, Jina la Yesu na ufunuo.

⁶¹ Tunaona ya kwamba hiki kilikuwa kimetiwa Mihuri Saba, na kila Muhuri ulikuwa umefungwa kukizunguka. Na ufunuo unapokuja, Yeye alivuta Muhuri, akaufungua huu na kusoma yale Muhuri huo uliyosema. Kisha akafungua huo mwingine, lile gombo, na kusoma uliyosema Muhuri huo. Akaufungua huo uliofuata, akautoa na kuona yale Muhuri huo uliyosema, na kwamba ufunuo ulikuwa ni nini. Hivyo ndivyo hasa vile Mihuri yetu Saba, tutakayoingilia karibuni, tunatumaini, itakawa hivyo. Kila Muhuri, wakati unapoondolewa kwenye kile Kitabu, utafunguliwa, nao utaonyesha yale hasa yaliyotukia.

⁶² Tunaona ya kwamba kuna “saba,” tano katika mpango wa ukombozi. Tano ndiyo namba hiyo. Na kuna tano saba; Mihuri Saba, Roho Saba, malaika saba, Baragumu Saba, na nyakati saba za kanisa. Kwa hiyo, unaona, hizo saba tano ni neema. Tano ni neema, na saba ni ukamilifu. Kwa hiyo inakubaliana kikamilifu tu kabisa, unaona. Vema.

⁶³ Kama vile, kila Muhuri unaovunjwa katika Neno la Mungu, unamfunulia huyo mtu wa wakati huo, ni wakati gani tunaoishi, roho ya wakati huo, kanisa la wakati huo. Ufunuo 10, mwishoni, tunaona wakati ule Muhuri wa mwisho ulipovunjwa, tunamwona yule Malaika amesimama ameweeka mguu mmoja juu ya nchi, na huo mwingine juu ya bahari, ameinua mkonono Wake kuelekea Mbinguni, na upinde wa mvua juu ya kichwa

Chake, akiapa kwa Yeye aliye hai milele na milele, ya kwamba wakati umekwisha, wakati ule Muhuri wa mwisho. Nanyi ngojeni mpaka tutakapoifikia ule Mihuri na kuona mahali huo Muhuri ulipo. Baada ya kupata yale majuma sabini, halafu tutaona mahali ilipo ile Mihuri, "Wakati umekwisha," ukombozi umekwisha, Yeye sasa ni Simba na Hakimu. Yeye ni Mwokozi wako asubuhi ya leo, lakini siku moja atakuwa Hakimu wako.

⁶⁴ Ya 8 hadi ya 1...aya ya 14 ya sura ya 5, inafunua wakati wa kuabudiwa kwa Mwana-Kondoo, Mbinguni na duniani pia; kile Kitabu kilichotiba Muhuri saba, yule Mwana-Kondoo aliyestahili, Mkombozi wa Jamaa. Na kutoka aya ya 8, hadi ya 14, Malaika wanamwabudu Yeye, wazee wanamwabudu, wale Wenyewe Uhai wanamwabudu. Na Yohana akamwabudu sana hatia akasema, "Kila kiumbe Mbinguni, duniani, chini ya nchi, kilisikia nikisema, 'Baraka, utukufu, nguvu, hekima, ina Mwana-Kondoo.'" Ni wakati wa kumwabudu yule Mfalme Mwana-Kondoo. Sasa, Kanisa limeondoka, kumbukeni.

⁶⁵ Sasa hebu na tufungue Danieli, na sura ya 9, na aya ya 1 hadi 3. Na halafu tutachukua 20 hadi 27, kwa sababu haya ni maombi tu ya Danieli. Ninawatakeni mrudie kusoma hii tena na tena, juma nzima, sasa, mpaka mtakapolipata.

*Katika mwaka wa kwanza wa Dario, mwana wa...
wa uzao wa Wamedi, aliyetawazwa kuwa mfalme juu
ya ya milki ya Wakaldayo;*

*Katika mwaka wa kwanza wa kumiliki kwake,
mimi Danieli,...-fahamu, nilifahamu kwa kuvisoma
vitabu, nilifahamu hesabu...miaka, ambayo neno la
BWANA lilimjia Yeremia nabii, ya kuutimiza ukiwa wa
Yerusalem, yaani, miaka sabini.*

*Sasa (inayofuata) Nikamwelekezea Bwana Mungu uso
wangu, ili kutaka kwa maombi, na dua, pamoja na
kufunga, na kuвая nguo za magunia na majivu.*

Nikamwomba BWANA, Mungu...nikaungama,...

⁶⁶ Na anazidi kuendelea mbele, mpaka sasa tunafikia aya ya 20. Ili kuokoa wakati, watu wakiwa wamesimama, ninataka mfikie kwenye aya ya 20, mpaka tutakopofikia sasa kwenye—kwenye aya ya 20.

*Basi hapo nilipokuwa nikisema, na kuomba, na
kuiungama dhambi yangu, na dhambi ya watu wangu
Israeli, na kuomba dua yangu mbele za BWANA, Mungu
wangu, kwa ajili ya mlima mtakatifu wa Mungu wangu;*

*Naam, nilipokuwa nikinena katika kuomba, mtu
yule, Gabrieli, niliyemwona katika njozi hapo kwanza,
akaanza,...akirushwa upesi, alinigusa panapo wakati
wa dhabihu ya jioni.*

Akaniagiza, akaongea nami, akasema, Ee Danieli, nimetokea sasa, ili nikupe akili upate kufahamu.

⁶⁷ Laiti tungalikuwa pale! Yeye alimkuta akiwa vipi? Katika maombi.

Malaika, “mtu yule.” Unaona, alimwita Yeye, “mtu yule.” Na akiwa wa . . .

Mwanzo wa maombi yangu ilitolewa amri, (naye akaja ili apate kwenda) nami nimekuja kukupasha habari; maana wewe unapendwa sana; kama . . . basi itafakari habari hii, na kuyafahamu maono haya.

Muda wa majuma sabini umeamriwa juu ya watu wako, na juu ya mji wako mtakatifu, ama mji wako, ili kukomesha makosa, . . . kuishiliza dhambi, na kufanya upatanisho kwa ajili ya uovu, na kuleta haki ya milele, na kutia muhuri maono na unabii, na kumtia mafuta yeye aliye Mtakatifu.

Hizo hapo sababu sita za kuja Kwake. Sasa angalia.

Sasa, basi ujue na kufahamu, (sasa sikiliza) ya kuwa tangu kuwekwa amri ya kutengeneza na kuujenga upya Yerusalem hata . . . Masihi aliye mkuu; kutakuwa na majuma saba; . . . katika majuma sitini na mawili utajengwa tena pamoja na njia kuu zake na handaki, naam, katika wakati wa taabu.

. . . baada ya yale majuma sitini na mawili, Masihi atakatiliwa mbali, lakin si kwa ajili yake mwenyewe: na watu wa mkuu atakayekuja—mkuu atakayekuja, watauangamiza mji, na patakatifu; na mwisho wake utakuwa pamoja na gharika, . . . na hata mwisho ule vita vitakuwako; ukiwa umekwisha kukusudiwa.

Naye atafanya agano thabiti (sikilizeni) na watu wengi kwa muda wa juma moja; moja la haya majuma sabini: na kwa nusu juma hiyo ataikomesha sadaka na dhabihu; na mahali pake litasimama chukizo la uharibifu; na hivyo, hata ukomo, na ghadhabu iliyokusudiwa imemwagwa juu yake mwenyewe kuharibu.

⁶⁸ Sasa, hilo hapo somo letu kwa mikutano mingine mitatu, minne, mitano ifuatayo, lo lote atakalofunua Bwana. “Majuma sabini.”

⁶⁹ Sasa, nitamwomba Dok, kama akiweza, usiku wa leo, kuweka ubao wangu pale, ili kwamba nitaweza kuyachora. Sitaki mlakose. Sasa hamna budi kusoma pamoja nami, na kusoma kindani, la sivyo litawapita. Nami ninataka kuyachora hapa kwenye ubao, halafu nanyi mlele penseli zenu na karatasi na mwandike tarehe hizi, nyakati hizi, na mambo yote kuhusu jambo hilo.

⁷⁰ Sasa, yale majuma sabini yanaanza (sasa shikeni jambo hili) baada ya kanisa kuondolewa. Sasa, kila mtu anayelielewa jambo hilo, aseme, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa, baada ya Kanisa kuondolewa.

⁷¹ Ufunuo 6:1, mpaka Ufunuo 19:21, inahusika na yale majuma sabini, kwa hiyo hatuna budi kusimama na kuelezea, kabla hatujaendelea mbele zaidi. Hatuna budi kusimama na kuelezea ni kwa nini majuma haya sabini. Maana, kama hatuyaelezei, Mihuri itawapita, mtapitwa na hizo Baragumu, mtapitwa na hivyo Vitasa, hayo Mapigo, hizo roho chafu kama chura, hizo Ole tatu, kule kutupwa kwa lile joka jekundu, yule mwanamke katika jua. Mtayakosa yote, msipoyafahamu, maana yanatendeka papa hapa katika juma hili la sabini. Hapo ndipo yanapotukia.

⁷² Sasa, nabii Danieli alikuwa huko Babeli kwa miaka sitini na minane. Ninyi mnaotaka kufuatia kufuatia marejeo nyuma, na kujiokolea wakati kidogo, jambo ambalo ilinibidi ku-kulitafuta. Miaka sitini na minane! Yeye alienda uhamishoni katika 606 K.K., na wakati hilo ono lilipomtokea ilikuwa ni—ni 538 K.K. Ukitoa 538 kutoka 606, inabakia sitini na minane. Alikuwa Babeli miaka sitini na minane, mionganoni mwa makafiri, na hata hivyo alipata ushindi. Amina. Sisi hatuwezi kukaa hata saa moja.

⁷³ Lakini yeye alikuwa katikati kabisa, bila mtu mwingine ye yote isipokuwa wenzake watatu, na hao walikuwa katika sehemu mbalimbali za ule ufalme. Lakini, Danieli, akisimama peke yake na Mungu, alidumisha ushindi kwa muda wa miaka sitini na minane. Wazia jambo hilo! Sitaki kuanza kuhubiri, kwa sababu huu unapaswa kuwa ni Ujumbe wa mafundisho. Lakini, kwa muda wa miaka sitini na minane, yeye alikuwa amedumisha ushindi wala hakuwa ametiwa unajisi, mbele ya Mungu; bila ubatizo wa Roho Mtakatifu, bila Damu ya Yesu Kristo kumfanyia upatanisho; akiwa na damu ya mafahari tu, na mbuzi, na mitamba, ambayo ilimbidi kuwatoa sadaka kwa siri, kwa sababu ya desturi za makafiri wa nchi ile. Walikuwa wamechukuliwa kule chini. Yeremia aliwatabiria, ya kwamba walikuwa wanaenda huko.

⁷⁴ Sasa, Danieli, loo, jamani, alikuwa ameanza kuona ya kwamba wakati ulikuwa unakaribia, kama vile tu tulivyo leo. Danieli alianza “kufahamu,” akasema, “kwa kuvisoma vitabu.”

Katika mwaka wa kwanza wa kumiliki kwake, . . . Danieli, . . . katika kumiliki kwake, mimi Danieli, nilifahamu kwa kuvisoma vitabu, nilifahamu hesabu ya miaka, kwa hiyo . . . neno la BWANA lilimzia Yeremia nabii, ya kutimizwa miaka sabini katika . . . ukiwa wa Yerusalemu.

⁷⁵ Yeremia, katika 606 K.K., alitabiri, kwa sababu ya dhambi zao na ukafiri, ya kwamba wangekuwa huko miaka sabini.

⁷⁶ Mnakumbuka, kulikuweko na nabii mwингine aliyejitokeza siku hiyo. Siwezi kukumbuka jina lake kwa wakati huu. Huenda nikaweza kulikumbuka kwa ajili yenu mnamo—mnamo dakika chache, kama ningerejea nyuma kidogo. Lakini ye ye aliкуja na kusema, “Yeremia, umekosea. Mungu atawaweka Israeli kule kwa siku kadha tu, kwa ninii kadha, kama miaka miwili.”

⁷⁷ Yeremia akasema, “Na iwe hivyo. Amina.” Yeye akasema, “Lakini ngoja kidogo. Hebu mimi na wewe tuchunguze mambo, kama manabii.” Akasema, “Kumbuka, kuna hao amba walitabiri mbele yetu, na kusema mambo ya uongo. Na Mungu aliwapatiliza kwa kusema mambo ya uongo. Kwa hiyo, hebu tuwe na uhakika. Lakini Bwana Mungu ameniambia kungali kuna miaka sabini bado.”

Mungu alimpiga nabii yule wa uongo, na kuondoa uhai wake mwaka uo huo, kwa maana Mungu alikuwa amemwambia nabii huyu wa kweli ya kwamba kulikuweko na miaka sabini.

⁷⁸ Nami nawatakeni mwone vile Danieli, ingawa alikuwa ni mgeni, ingawa alikuwa ameondolewa kwa watu wake, ameondolewa kanisani mwake, bila ya ibada hata moja ya kanisa, bila kanisa lo lote la kuhudhuria, bila nyimbo zo zote za kuimbwa ila zile alizoimba mwenyewe, katikati ya mambo haya yote, angali alishikilia yale aliyo sema nabii yule. Amina! Amina!

⁷⁹ Hana kanisa la kuhudhuria, hana mtu wa kushiriki naye; kila mtu alihudhuria mahekalu ya makafiri, kila mtu aliabudu sanamu zake. Hakuna nyimbo za Kikristo; hakuna mtu aliyeamini jambo lile lile aliloamini. Na katika miaka sitini na minane, tangu alipokuwa mvulana mdogo wa kama umri miaka kumi na miwili, kumi na minne, wakati alipochukuliwa akapelekwa kule, ye ye alidumu kuwa mwaminifu kwa Mungu; na akafahamu kwa nabii Yeremia ya kwamba siku zili kuwa karibu kutimia.

Jinsi vile jambo hilo lingutahadharisha moyo wa nabii ye yote wa kweli wa Mungu leo, kwamba tuangalie nyuma tuone yale nabii huyu wa kweli aliyo sema, na tujue ya kwamba tuko katika wakati wa mwisho.

⁸⁰ Akasema, “Nilifahamu kwa kuvisoma vitabu ya kwamba Yeremia, ndugu yangu, miaka mingi, mingi iliyopita, alitabiri ya kwamba Israeli wangekaa huku kwa muda wa miaka sabini. Na wakati huo uko karibu kutimia.” Ndipo akajitayarisha. Akafunga, na kujitakasa, na wakati aliponinii... majivu na nguo za magunia, na kuyaweka kichwani mwake, naye akaingia kwenye kufunga na kuomba, apate kufahamu kwamba ni siku gani walikuwa wanaishi.

⁸¹ Na kama Danieli, nabii wa Bwana, aliweza kuvichunguza vitabu nya Yeremia, na vikamfikisha mahali kama hapo; ya kwamba hata kule kutoka kwa Israeli, wote wakiwa hai, walikuwa wanatoka Babeli, kwenda kwenye nchi ya uenyeji wao, kungemfanya kufunga kwa nguo za magunia na majivu. Ni zaidi sana viyi inavyolipasa Kanisa la Mungu aliye hai kufanya hivyo, kujua ya kwamba wakati unaisha na hautakuweko tena; na kule Kuja kwa Bwana Yesu Kristo, na ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu uko tayari kuanza! Tunawezaje kupidisha wakati bure, kucheza kamari, kwenye vidimbwi nya kuogelea Jumapili, hatuna wakati kwa ajili ya Bwana? Kwenda tu huko... Kama mchungaji akisema kitu juu ya jambo fulani ama lingine ambalo mtu hupendi, unaamka na kutoka. Na kama ninii—kama kanisa likichukua muda mrefu sana, mbona, wewe—wewe, una—unachukia. Angalia hali yetu. Angalia tunayoyafanya.

Linganisha maisha yetu na ya nabii yule. Mtu mmoja, katika ufalme mzima, bila kanisa la kuhudhuria, wala hakuna lingine mahali po pote angalihudhuria. Yalikuwa yamebomolewa na kuchomwa moto; mji wake, watu wake walikuwa mateka. Miaka sitini na minane! Sitini na minane, sitini na tisa, sabini; alikuwa na miaka miwili iliyosalia. Kwa hiyo alipoanza kusoma katika kitabu na kuona ya kwamba wakati ulikuwa unakaribia kutimia, kutimizwa, alimwendea Mungu katika maombi, apate kujua jambo hilo.

⁸² Ni wakati wa jinsi gani! Tunafanya nini? Wakati, “Mataifa yanavunjika; bahari inavuma; mioyo ya watu inavunjika kwa hofu; mshangao wa wakati.” Mambo haya yote, maandishi kwenye ukuta. Ubaguzi wa rangi; kila namna ya maovu yanaendelea ulimwenguni; na kuzozana, na kupigana, na ghasia. Na zana za vita zikining’inia kwenye mabanda, ambapo taifa moja dogo ukubwa wa Cuba hapa chini linaweza kuuangamiza ulimwengu katika dakika kumi. Nao wakizozana mmoja kwa mwagine, makafiri wasiomjua Mungu wala hawazui nguvu zake.

Na Roho Mtakatifu Kanisani, akitenda kazi kati ya Walioteuliwa, akijionyesha kwamba Yeye yu hai baada ya muda wa miaka elfu mbili, ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Tunawezaje kuketi kivivu? Tunawezaje kulivuka jambo hilo vivi hivi? Wakati umewadnia wa kujiweka sawa, tukiitazamia ile saa kuu inayokuja.

⁸³ Sasa, yeye alisoma katika Yeremia, sura ya 25, hebu na tufungue Yeremia, sura ya 25, na tusome yale aliyosema Yeremia. Kwa kweli, hebu na tuanzie kwenye aya ya 8, maana ni... Ninawatakeni mwe na hakika ya kupata jambo hilo. Aya ya 11 ndipo nilipokuwa nimeandika hapa chini nipate kusoma, lakini hebu na tuanzie kwenye aya ya 8.

Basi BWANA wa majeshi asema hivi;...

Ninapenda tu jambo hilo. Wakati ninapoweza kumsikia nabii akisimama akiwa na BWANA MUNGU ASEMA HIVI, ndugu, ndivyo ilivyo. Kwangu mimi, hilo linatosha. Ni hayo tu.

...BWANA wa majeshi asema hivi; Kwa kuwa hamkuyasikiliza maneno yangu,

Angalieni, nitapeleka watu na kuzitwaa jamaa zote za upande wa kaskazini, asema BWANA, nami nitatumua ujumbe kwa Nebukadreza, mfalme wa Babeli, mtumishi wangu, nami nitawaleta tena...juu ya nchi hii, na juu yao wakao ndani yake, na juu ya mataifa haya yote yaliyopo pande zote; nami nitawaangamiza kabisa,...

Kumbukeni, hao walikuwa ni wateule wa Mungu ambao Yeye ananena habari zao. Hao hawakuwa ni makafiri. Hao walikuwa ni wafuasi wa kanisa.

Tena, nitawaondolea sauti ya kicheko,...na sauti ya furaha, (kama tulivyo nayo leo, rumba zote, Ricky na Elvis,) na, lo, sauti ya bwana arusi,...sauti ya ndege... ama, bibi-arusi, hasa, sauti ya jiwe la kusagia,...na nuru ya mishumaa.

Na nchi hii yote pia itakuwa ukiwa,...

Msikie nabii huyo akilia kwa sauti kuu, "Nchi hii yote itakuwa ukiwa!" Wala si kumwiga mtumishi huyu mkuu wa Mungu, lakini ninatabiri ya kwamba taifa hili lote litakuwa ukiwa. Mungu ataliadhibu taifa hili kwa ajili ya dhambi zake. Kama Mungu hangewaacha israeli, wateule Wake, Uzao wa Ibrahim, ambao alifanya agano na ahadi nao, kama Yeye hangewaachilia kwa kufanya uovu; ingawa walikuwa wanadini kweli kweli moyoni, walikuwa na makanisa makubwa, na makuhani, na waalimu; lakini kwa sababu ya uzinzi na kadhalika mionganoni mwao, na Mungu akawafanya wavune waliyopanda, vivyo hivyo na sisi tutajuta pia. Aya ya 11:

...nchi hii yote itakuwa ukiwa, na kitu cha kushangaza;..

Hiyo ni kusema, kila mtu ataangalia tu na kusema, "Hao hapo. Walikuwa watu wakuu sana. Waangalie sasa."

...nayo mataifa haya watamtumikia mfalme wa Babeli miaka sabini.

Huo ni muda wote wa maisha. Hapo ndipo wakati mama yako mzee, mama mzee mbarikiwa alipokuwa mtoto mchanga. Walikuwa kule bila Mungu, bila kanisa, bila wimbo, bila cho chote kile, kwa kizazi kizima, mpaka kizazi hicho chote chenyeye kutenda dhambi kilipokufa.

Na itakuwa miaka hiyo sabini itakapotimia, kwamba nitamwadhibu mfalme wa Babeli, na taifa lile, asema BWANA, kwa sababu ya uovu wao, nayo nchi ya Wakaldayo pia; nami nitaifanya kuwa ukiwa wa milele.

*Nami nitaleta juu ya nchi ile maneno yangu yote
niliyoyanena juu yake, naam, yote yaliyoandikwa ndani
ya kitabu hiki, aliyotabiri Yeremia juu ya taifa lote.*

*Kwa maana mataifa mengi na wafalme wakuu
watawatumi kisha—watawatumi kisha; naam, hao pia;
nami nitawalipa... kwa kadiri ya matendo yao, na kwa
kadiri ya maneno ya mikono yao.*

*Maana BWANA, Mungu wa Israeli, aniambia
hivi, Pokea kikombe cha divai ya ghadhabu hii
mkononi mwangu, ukawanyweshe mataifa yote, ambao
nitakupeleka kwao.*

Kwa maneno mengine, “Yeremia, nimekupa ujumbe huu. Usiketi kitako. Usikae mahali pamoja, lakini watabirie mataifa yote.” Mnalifuata? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] “Tabiri kwa taifa lote. Onyesha ishara Zangu na maajabu, na uwafanye wajue ya kwamba Mimi ninakuja kufanya jambo hili.”

*Nao watakunywa, na kulewa-lewa, na kufanya
wazimu, kwa sababu ya upanga nitakupeleka kati
yao.*

⁸⁴ Wao wanafanya nini katika siku hii hii tuishiyo sasa hivi? Wanakuuta na—nabii wa uongo, wanakuuta mwe-mwenye kupatana, wanakuuta m—mshupavu wa dini, mpiga ramli, ama mwotaji wa ndoto, ama namna fulani ya mwenye kushirikishana mawazo. “Wataenda wazimu!” Na neno *wazimu*, kama utalivunja-vunja, linamaanisha “kichaa.” “Kwa kweli wataingia kichaa, na, kusema, ‘A-ha, msimjali huyo mtakatifu anayejifingirisha, huo upuuzi,’ kwa sababu ya Neno nitakalowapelekeea.”

⁸⁵ Mnaona historia ikijirudia yenye? Yeremia hangekubaliana na Mafarisayo wao, Masadukayo, Maherodia, wo wote wale. Yeye, yeche alilitoa tu Neno, nalo likawafanya wamkasirikie sana. Kitu gani? Sasa angalia.

*Ndipo nikakipokea kikombe kile mkononi mwa
BWANA, nikawanywesha mataifa yote,...*

Yeremia hakukaa nyumbani. Yeremia hakukaa tu katika mahali pamoja, lakini aliwanywesha mataifa yote,

... ambao BWANA alinipeleka kwao;

⁸⁶ Yeremia alilichukua Neno la Bwana, divai ya Neno Lake. Na divai ni nguvu za Neno Lake. Divai ina nguvu. Divai ni kileo. Divai ina nguvu nyuma yake. “Nami mimelichukua Neno la Bwana,” kasema Yeremia, “na kulidhihirisha. Divai, zile nguvu zilizo ndani Yake, nilizithibitisha mbele zao, wala hawangeskia Hilo.”

Mungu akasema, “Basi nitawapeleka Babeli kwa muda wa miaka sabini.” Hivyo ndivyo alivyofanya hasa. Wenye haki na wasio haki walienda, wote pamoja.

⁸⁷ Sasa, turudi kwenye lile somo. Danieli alikuwa akisoma. Wazia tu, Danieli alisoma maneno yale yale tunayosoma asubuhi ya leo. Danieli alisoma Biblia ile ile, vituo vile vile, sentensi zile zile, mambo yale yale ambayo mimi ninaamini, kwa neema ya Mungu, nitawasomea katika Jumbe chache zifuatazo, jambo lile lile, kuwaonyesha ya kwamba tuko katika wakati wa mwisho.

Naye Danieli, akilichukua Neno kutoka kwa Yeremia, anashuka anaenda kule Babeli. Naye alikuwa nabii aliyetiwa mafuta. Ndipo akafanya miujiza, ishara, aliweza kufasiri lugha zisizojulikana, na kufanya ishara na maajabu mionganoni mwao. Hata hivyo, akisimama peke yake, akiwa peke yake! Amina! Alisimama peke yake.

⁸⁸ Lakini Yeremia alikuwa ameandika Maneno haya miaka mingi, mingi sana hapo kabla. Na Danieli, akifasiri hilo Neno, akapata . . . “Aisei, ngoja kidogo. Tunakaribia wakati wa mwisho, kwa maana tayari tumeshakaa huku miaka sitini na minane. Na nabii wa Bwana,” amina, “ndugu yangu, nabii wa kweli wa Mungu aliyejithibitisha kwamba ni nabii, alitutabiria. Nimeliandika hapa katika kitabu, kilichosema, ‘Itatimizwa miaka sabini.’ Ee Bwana Mungu, tunakaribia mwisho. Kizazi chote kile kimekwisha. Utafanya nini sasa, Bwana? Uliahidi kututumia . . .” Naye akajiandaa, kusudi apate kuomba.

⁸⁹ Ee Mungu, kama kuliwahi kuwa na wakati ambapo tunapaswa kujiweka tayari, kuomba, ni sasa. Kwa kuwa, sisi kama mtumishi Wake wa kweli, tunaona, kwa Nyarakaa za mtume, kwa maonyo ya Roho Mtakatifu, ya kwamba tuko katika siku ya mwisho. Roho Mtakatifu ananena jambo Hilo. “Katika siku za mwisho, watu watakuwa wakaidi, wenyewe kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizua, wasiowapenda walio wema.” Ninafahamu kwa Waraka.

⁹⁰ Nami ninafahamu ya kwamba watakuja wenyewe kudhihaki, katika siku ya mwisho. Nafahamu ya kwamba taifa litakuwa litapigana na taifa, katika siku ya mwisho. Nafahamu ya kwamba kutakuweko na misukosuko ya mawimbi, katika siku ya mwisho. Ninafahamu ya kwamba kutakuweko na vitu vya kutisha, kama visahani virukavyo, mbinguni, mambo ya ajabu yasiyoeleweka, na miyo ya watu ikivunjika kwa hofu. Kutakuwa na mishangao ya wakati, na dhiki mionganoni mwa watu. Ninasoma ya kwamba wote wataingia katika mashirika na madhehebu, na watakuwa na muungano, katika siku ya mwisho. Nafahamu ya kwamba wanawake watakata nywele zao katika siku ya mwisho. Nafahamu watavaa nguo fupi, na kutembea kwa viatu vyenye visigino virefu, wakiliza njuga, katika siku ya mwisho. Ninafahamu ya kwamba uadilifu utakuwa duni sana katika siku ya mwisho. Nafahamu ya kwamba wahubiri watakuwa wachungaji wa uongo katika siku ya mwisho, ambao watapatana, wala hawatawalisha watu Neno la Mungu, ila

watazifuata kanuni za imani na kadhalika, badala yake. Lakini nafahamu kutakuweko na Sauti itakayokuja katika siku ya mwisho, ikilia kutoka nyikani, ikiwaita watu waurudie Ujumbe wa asili, wayarudie mambo ya Mungu. Nafahamu, kwa Kitabu, mambo hayo yatatukia.

⁹¹ Nafahamu ya kwamba katika siku za mwisho itakuja njaa. Makanisa yatakuwa yamejiweka katika utaratibu sana, na makavu sana na kila kitu, ya kwamba wakati wa mwisho itakuja njaa, wala haitakuwa ya chakula wala maji peke yake, bali ya kusikia Neno la kweli la Mungu. Na watu wataenda kutoka mashariki, kutoka magharibi, kutoka kaskazini, na kutoka kusini, wakitafuta kulisikia Neno la kweli la Mungu. Lakini makanisa yatakuwa yamejifanyia taratibu sana na magumu sana, hata watashindwa kulisikia Hilo. Nafahamu mambo hayo kwa Vitabu. Lakini, katika siku hiyo, Ee Mungu, kutakuwa na Tawi litakaloinku kutoka kwa Daudi.

⁹² Nafahamu ya kwamba Yeye atampeleka Eliya kabla hajaja ile siku wakati wa mwisho, naye atakuwa na Ujumbe ambao utaigeuza miyo ya watoto iwaelekee baba zao, kuwageuza kuelekea lile la asili, kurudi tena huko mwisho, na kuanza. Ninafahamu ya kwamba jambo hilo litatukia kabla tu Roho hajaliacha kanisa la Mataifa, kuwarudia Wayahudi.

⁹³ Wala sifahamu tu hayo kwa Waraka tu. Ninafahamu kwa Neno, kwa Neno lililoandikwa, ya kwamba Israeli watarudi kwenye nchi ya Uenyeji wao; nami ninawaona wakirudi.

⁹⁴ Ninafahamu kwa Nyaraka, za manabii, ya kwamba Israeli watakuwa taifa. Wataanzisha tena kuabudu hekaluni. Mungu ataanza kumshughulikia tena wakati atakapoingia katika nchi ya uenyeji wake. Loo! Manabii wawili watainuka katika siku za mwisho, pamoja nao. Nafahamu jambo hilo. Mara tu Kanisa la Mataifa litakapoondoka, manabii wawili watasasili, Elisha na Musa, huko Israeli. Tutalipata tutakapoyapitia.

⁹⁵ Nabii aliona wakati ulikuwa karibu kutimia kule chini huko Babeli. Vema.

⁹⁶ Gabrieli anatokea, kufunua si yale tu aliyokuwa anauliza, bali kumwambia ye ye yote yale yaliyokusudiwa kwa taifa la Kiyahudi, ya njiani mwote hata mwisho wa dahari. Amina! Yeye aliuliza jambo dogo, naye akapata jambo zima. Aliuliza tu apate kujua...

⁹⁷ Danieli alikuwa anajaribu kupata habari, "Hata lini, Bwana, itachukua muda gani zaidi sasa? Yeremia nabii, mtumishi Wako, ndugu yangu, ametabiri miaka sitini na minane iliyopita, na kusema, 'kuna miaka sabini ambapo watu hawa watacaa huku.' Kile kizazi cha kale karibu kimekwisha sasa."

⁹⁸ Kuna kizazi cha kale cha kipentekoste kilichoinuka, miaka arobaini iliyopita. "Wapiganaji wa kale," ndivyo walivyoitwa. Waliunda madhehebu, na kupigana, na kuzozana, njia nzima

kupita Mlima Horebu na Nebo, kupertia kote kule. Lakini, hatimaye, tuko mtoni sasa. Yeye atainua kipyä, pamoja na Yoshua apate kuwavusha. Torati ilishindwa; Musa aliondoka nayo; Musa alishindwa. Yoshua akawavusha. Tunaona ya kwamba madhehebu yameshindwa, lakini Roho wa Mungu... Yoshua, neno *Yoshua*, maana yake ni “Yesu Mwokozi wetu.” Hilo, Roho Mtakatifu ataingia Kanisani. Si madhehebu, lakini Roho Mtaktifu atakuja kwa watu na kumfanya tayari kwenda juu, kuvuka Yordani. Ninafahamu kwa kukisoma Kitabu ya kwamba hayo ndiyo yatakayotukia. Na Mungu anajua hayo ndiyo ninayotafuta sasa, nipate kuwafariji watu Wake na kuwaambia mambo yaliyo karibu kutimia, hapa asubuhi ya leo, na pia huko nje katika nchi ambako kanda hizi zitakwenda, kila mahali ulimwenguni, ya kwamba tuko katika wakati wa mwisho.

⁹⁹ Yeye aliufunua wakati wote mpaka Ufalme uliporudishwa kabisa na ule Utawala wa Miaka Elfu ukaanza. Huo ndio uliokuwa Ujumbe wa Gabrieli. Yeye alisema, “Nimekuja kukwambia ya kwamba kuna miaka sabini, majuma sabini, bado, yaliyoamriwa juu ya watu wako, yaliyoamriwa hata mwisho wa kizazi cha Wayahudi. Kuna majuma sabini.” Sasa angalia yale aliyosema Yeye. Ya kwamba sasa, tangu kuwekwa amri ya kuujenga upya...

Muda wa majuma sabini umeamriwa juu ya watu wako, na juu ya mji...

“Mji wako.” Babeli haukuwa mji wake. Ambaye... Mji wake ulikuwa wapi? Yerusalem.

¹⁰⁰ Sasa, wakati tutakapofikia kwenye—kwenye ninii ya saba, ama kule kuthibitishwa mara sita, tuona mji huo ni upi, na kulileta na kuthibitisha alikuwa ni nani, ni nani aliyeuanzisha, mahali ulipotoka. Utadumu muda gani? Utajengwa tena? Katika wakati gani? Loo, mambo makuu yanatungojea. Vema.

Muda wa majuma sabini umeamriwa juu ya watu wako, na juu ya...mji wako,...ili kukomesha makosa,...

Sasa, Yeye kamwe hakusema, “Danieli...” Hapana shaka ila alimwambia ya kwamba majuma sabini yalikuwa... ninamaanisha miaka sabini ilikuwa karibu kumalizika. Sitini na minane, ilisalia miaka miwili pekee. Nasi tunaona ya kwamba unabii wa Yeremia ultimia kikamilifu kabisa. Miaka miwili baadaye, wakatoka. Nehemia akaenda akapata amri kutoka kwa mfalme, akaujenga ukuta katika wakati wa shida. Walifanya kazi. Alisema, “Ukuta...” Sikilizeni jambo hili.

...ili kukomesha makosa,... kuishiliza dhambi,...

“Kuishiliza dhambi.” Kwa nani? Wayahudi. “Umeamriwa juu ya watu wako,” si juu ya Mataifa. “Juu ya watu wako,” Wayahudi. “Na mji wako,” si New York, si Boston, Philadelphia,

Chicago, Los Angeles, Rumi. Lakini, “Juu ya mji wako,” Yerusalem.

...kasema ili kukomesha makosa, . . . kuishiliza dhambi, . . . kufanya upatanisho kwa ajili ya uovu, na kuleta haki ya milele, na kutia muhuri maono na unabii, na kuntia mafuta yeche aliye Mtakatifu sana. (Angalia!)

Basi ujue na kufahamu, ya kuwa tangu kuwekwa amri ya kutengeneza na kujenga upya Yerusalem (ambao ulikuwa ndio mji wake) hata . . . Masihi Aliye Mkuu; kutakuwa na majuma saba (ya yale sabini).

¹⁰¹ Ngojeni mpaka tutakopofikia jambo hilo! Loo, jamani! Hiyo ni baraka ambayo mimi . . . Nitachukua kamba nijifungie mahali hapa.

¹⁰² Akafunua mambo yote yajayo, kasema, “Sitakwambia tu sasa ya kwamba miaka hiyo miwili iko karibu kuninii, bali itamalizika, itatimizwa.” Nasi sote tunajua ya kwamba wao walikaa kule miaka sabini kamili, kisha—kisha wakatoka, sawasawa kabisa tu na vile nabii alivyo sema. Na Isaya, ama ninamaanisha . . . Danieli alimwamini nabii huyo, kwa hiyo huyu hapa, tayari. Vema. Naye akaninii . . .

¹⁰³ Na sasa, wakati Gabrieli alipokuja, alisema, “Nimekuja kukuonyesha mambo yote, kukufunulia mambo haya, ya kwamba, yote mpaka mwisho.” Mnaona? Angalia.

...chukizo la uharibifu hata ukomo, na ghadhabu iliyokusudiwa imemwagwa juu yake . . .

¹⁰⁴ *Ukomo* ni “mwisho wa mambo yote.” “Nitawaonyesha yale yatakayotukia.” Sasa sikilizeni. Mnalipata! “Mimi . . . Danieli, nimetumwa. Umependwa sana Mbenguni. Nami niliyasi kia maombi yako na nimeshuka sasa kukwambia yale yaliyokusudiwa kwa ajili ya Wayahudi na Yerusalem, tangu sasa hivi mpaka mwisho wa ukomo, jambo lote.”

¹⁰⁵ Sasa, mnaelewa, darasa? Kama tunaweza kujua majuma haya sabini ni nini, tunajua mwisho ni lini. Loo, jamani! Mungu na atusaidie kuyajua. Inatuambia hasa mahali fulani katika kurasa hizi, kuto ka wakati ule hata wakati huu hasa, hata ukomo, wala haitakosea hata dakika moja.

¹⁰⁶ Jinsi Neno la Mungu liliyuo kuu . . . Wakati Mungu alipoiumba dunia na kuiweka katika mzunguko. Nami nilikuwa nikihubiri hivi majuzi usiku, Jumapili usiku, jinsi ambavyo hakuna kitu kinakosewa. Mbona, dunia hii inazunguka kikamilifu kabisa hata wao wanaweza kukwambia barabara jua na mwezi vitapita lini, katika miaka ishirini kuanzia leo, hata kufikia kwenvye dakika ile ile. Siwezi kuwaambia, kwa chombo cho chote cha majira saa tulicho nacho ulimwenguni; kitapoteza dakika mbili ama tatu kwa mwezi, ama kukimbia dakika mbili ama tatu, kile kizuri sana tulicho nacho. Hatuwezi kutengeneza kitu cho chote kilicho kikamilifu namna hiyo. Kwa

sababu, kuna kitu kimoja tu kilicho kikamilifu, hicho ni Mungu. Na Mungu na Neno Lake ni mmoja, kwa hiyo Neno la Mungu ni kamilifu.

¹⁰⁷ Na kama tunaweza kuzipata siku hizi, tutapata ukomo utakuwa ni lini hasa. Mnalifahamu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] “Limeamriwa hata ukomo.” Aya ya 24, “watu wako na mji wako mtakatifu,” ambao ni Yerusalem. Nina aya ya 21 . . . aya ya 24 hapa. Yesu alirejea kwenye jambo hili katika Mathayo 24.

¹⁰⁸ Sasa, Ndugu Collins, kama yupo hapa asubuhi ya leo, sijui kama yupo ama hayupo. Katika yale maswali hivi majuzi usiku, ye ye aliuliza swalii. (Nadhani ni sawa kwangu kusema jambo hili, Ndugu Collins.) Juu ya ““Chukizo la uharibifu,’ unaona, lilimaanisha nini?”

¹⁰⁹ Yesu alinena juu yake, katika Mathayo sura ya 24, nasi tunaona. Naam, Mathayo 24:15. Sasa hebu nilipate jambo hilo upesi sana, ili muwezi kuona kile, Yesu akizungumza juu ya jambo lile lile hapa, akirejea kwa Danieli. Mathayo 24:15, kwenu ninyi mnaoandika. Nawatakeni, kila mmoja sasa, hasa sana usiku wa leo na—na Jumapili ijayo, leteni penseli na makaratasi, ‘maana tutaninii . . . labda iwe una kinasasauti. 24, na aya ya 15, “Basi hapo . . .”

*Na hapo mtakapoliona chukizo la uharibifu, lile
lililonenwa na nabii Danieli, . . .*

Wazia! Hii ni miaka mia nne na themanini na mitatu, -nne, -tano, miaka themanini na mitano kabla.

. . . *nabii Danieli, limesimama katika patakatifu . . .*

Sasa angalia katika Biblia yako. Liko katika mabano.

. . . *(asomaye na afahamu)*

¹¹⁰ Sasa, Yeye anazungumza na Wayahudi. Wao wanataka kujuua, “Na hekalu hili je? Litabomolewa lini? Litajengwa upya lini? Itakuwa ni lini ambapo halitasalia jiwe juu ya jiwe? Itachukua muda gani?”

¹¹¹ Akasema, “Mtakapolioana ‘chukizo la uharibifu, limesimama wakati . . .’ Danieli, ‘limesimama katika patakatifu.’” Kasema, “Mtakapoona jambo hili likitimia, sasa asomaye na afahamu yale anayonena.”

Hiyo ndiyo sababu tunamwomba Mungu, alifanye jambo hilo kamilifu sana, hata hakutakuweko na kivuli cha mashaka. Kwa sababu, hatupaswi kuweka tafsiri yetu kwenye mambo hayo. Halina budi kuja kupitia BWANA ASEMA HIVI. Kwa hiyo, ninaliacha papo hapo mpaka nitakapofahamu.

Akamfunulia mambo yote, lile “chukizo.”

¹¹² Na, kumbukeni, lina maana mbili, kama tu vile, “Kumwita mwanangu kutoka Misri.” Kama vile Israeli walivyoitwa; vivyo hivyo na Yesu pia, Mwanawewe, aliiwa atoke.

Na jambo hilo litatukia kabisa, hakika kama ninavyosimama hapa. Naye alilifanya kwa njia fulani, Naye amelificha kabisa, amelificha lote kwa Kanisa. Loo, tutakapofikia jambo hilo, kwenye huo ufahamu wenyе sehemu sita, jinsi Yeye alivyoyaficha yote haya kwa Kanisa; ili kwamba Kanisa liwe likikesha kwa hilo kila dakika, halikujuu lini Yeye atakapokuja. Lakini sasa wakati wa Kanisa uko karibu na kwisha, kwa hiyo uko tayari kabisa kwa kule Kuja, linajifanya tayari tu.

¹¹³ Hili ni Andiko moja lililo muhimu sana katika kile Kitabu. Linafanya nini? Linatwambia juu ya kumalizika kwa wakati wa taifa la Kiyahudi, Wayahudi. Andiko hili, majuma sabini, linafunua na kuonyesha kikamilifu tangu wakati ambao Danieli alianzia kule, mpaka mwisho wa ule ukomo. Ni moja ya vyombo vikuu sana vya saa. Ni wangapi wamenisikia nikisema, “Kama ukitaka kujua ni siku gani ya juma, angalia kwenye kalenda. Ukitaka kujua tunaishi katika wakati gani, waangalie Wayahudi”? Hiyo ni kweli. Hiyo hapo kalenda ya Mungu, iliyotolewa kutoka papa hapa. Mwanatheolojia ye yote, mwanachuoni ye yote wa Biblia, mtu ye yote, atakwambia ya kwamba hawa ndio chombo cha kufahamia saa, Wayahudi.

Sasa tuna muda gani? Tunaninii tu... watu, joto, loo, mimi...

¹¹⁴ Halina uhusiano wo wote na Mataifa; hii Mihuri Saba, Mapigo Saba, Ole Saba, Baragumu Saba, hazina uhusiano wo wote. Kanisa la Mataifa litakuwa Utukufuni wakati huo. Halina uhusiano wo wote na sisi, Kanisa la Mataifa. Linawashughulikia Israeli tu. “Danieli, watu wako na Yerusalem.”

¹¹⁵ Sasa, na linafunua mambo ya kweli kwamba Mungu anawashughulikia Wayahudi wanapokuwa tu kwenye nchi ya unyejeji wao. Haleluya! Hapo ndipo ninapofikiri limefikia kiini chake, papo hapo.

Wao daima wanajaribu kulichukulia toka wakati ambapo Israeli walikuwepo kule katika wakati wa Danieli. Na mwandishi mmoja mashuhuri... Maana, ninajua baadhi ya wafuasi wake wako hapa, sitasema jambo hilo. Lakini hiyo ndiyo sababu wote walikuwa na upuuzi wote huu wa uongo.

¹¹⁶ Je, ulijua jinsi Wamileri, kabla hawajakuwa Wasabato, walilofanya kule? Katika mwaka wa 1919, walichukua mabawa yao, (nyote mliona jambo hilo kwenye gazeti la Courier), na wakapanda hapa juu wapate kuruka waende zao, asubuhi hiyo. Hiyo ilikuwa ni kuchukua majuma sabini ya Danieli. A-ha, Mmileri. Halafu, baadaye kidogo, wakiongozwa na Bibi Elen White, ambaye alikuwa ndiye nabii wao wa kike, wakageuka na kuijiita wenyewe Wasabato. Na sasa wamebadilisha jina lao

likawa Sauti ya Unabii. Unaona? Majina matatu mbalimbali ya madhehebu yale yale.

¹¹⁷ Sasa, lakini walikuwa wamekosea, kwa sababu walikuwa wakijaribu kuyaweka majuma hayo sabini kwa Wayahudi na Mataifa pia. Naye anasema hapa, “Ni kwa ajili ya watu wako.” Wala Mungu kamwe hajamshughulikia Myahudi akiwa nje ya Palestina. Na wakati Masihi, kwenye sabini, na mawili, alipokatiliwa mbali, (si kwa ajili Yake; kwa ajili yetu sisi, alipokatiliwa mbali), Israeli walitawanyika, wala (kamwe) hawajarudi kwenye nchi ya uenyeji wao mpaka katika miaka michache tu iliyopita. Kwa hiyo, wakati haukuhesabiwa pale kwa sababu ya wakati wa Kanisa. Mnalipata jambo hilo? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.]

Haingekuwa mwaka wa 1919. Ninaweza kuwaonyesha jambo lilitotukia katika mwaka wa 1919, lakini hapo ndipo wakati yule Malaika, ujumbe wa yule Malaika wa tatu ulipoanza na ile Ole ikaanza. Kweli kabisa. Lakini haikuwa ninii... Hapo ndipo vita vilipokoma kwa njia ya ajabu sana. Tunapata jambo hilo katika sura ya 7 tutakapolifiki, tutakapoifiki sura ya 7. Nyote mmenisikia nikihubiri jambo hilo, mara nyingi, mnaona, wakati ujumbe wa Malaika huyo uliposema, “Shikilieni pepo nne za dunia hata tutakapotatia muhuri Wayahudi, watumishi.” Na, sasa, waliendelea kungojea hata wakati wote wa Mataifa ulipokwisha.

Ndipo wakati Yeye aingiapo, basi—basi anawatia muhuri Wayahudi, wale mia na arobaini na nne elfu wanampokea Roho Mtakatifu. Hao hapo wale mia na arobaini na nne elfu, wametiwa muhuri. Ufunuo 7. Mmesoma jambo hilo.

“Ndipo nikaona hesabu kubwa sana iko Mbinguni tayari,” Yohana aliiona, “ya jamaa yote, lugha na taifa, nao walismama mbele za Mungu, wakiwa na mitende mikononi mwao, wamevikwa mavazi meupe, wakiimba. ‘Haleluya! Amina! Utukufu, hekima, heshima, uweza, nguvu, zina Mungu wetu milele na milele. Amina!’ wanasema kwa sauti kuu.”

¹¹⁸ Yohana hakuweza kufahamu wakati huo. Lakini aliangalia nyuma na akaona juu ya Mlima Sinai, (utukufu) wale mia arobaini na nne elfu ambao hawakutiwa unajisi na wanawake. Wayahudi! Wanawake, makanisa! Hawakuwa wamejiunga na madhehebu yo yote, Waluteri, Wamethodisti, Wabatisti, na Wapresbiteri. Lakini walikuwa ni Wayahudi tangu mwanzo, Othodoksi, nao walikuwa na hekalu lao pale, wakiabudu juu ya Mlima Sinai. Hao ni wale mia na arobaini na nne elfu. Hiyo ni baada ya haya; Kanisa limekwisha kwenda Utukufuni. Unaona?

¹¹⁹ Kwa hiyo, Bw. Smith alikosea, ilibidi akosee. Maana, utaliwekaje hilo hapa chini katika mwaka wa 1919, kuwatoa wale mia na arobaini na nne elfu? Ndipo umerudi kwenye fundisho la Waruseli tena. Unaona? Basi umerudi moja kwa moja

kwenye fundisho la Waruseli, ya kwamba, "Yesu alikuja mwaka wa 1914. Katika mwaka wa 1919 akalichukua Kanisa Lake. Na sasa Yeye ni mwili wa kisiri unaozunguka duniani, unafufua... unaenda kwenye kaburi la nyanya na babu, na kuwafufua wote, wote wale waliokuwa Waruseli." Upuuzi! Halina maana katika Neno. Halitakuja sawa. La, bwana. Halitakuja sawa.

¹²⁰ Lakini, Mungu ana Ukweli. Na Mungu Ndiye anayeweza kuifunua na kuiweka pale ndani, na kuionyesha kikamilifu, kwetu. Unaona? Ninaamini atafanya jambo hilo. Sijui. Ninawaambia Kweli. Sijui, lakini ninaamini. Ninaamini ya kwamba Yeye atafanya jambo hilo.

¹²¹ Kwa hiyo, unaona, Mungu hajawashughulikia Wayahudi. (Nawatakeni mweke jambo hili niani mwenu) mradi tu Israeli...

¹²² Hapo ndipo nilipojaribu kumwambia ndugu huyu anayeketi hapa, anayezungumza kuhusu kwenda Israeli, iacheni Israeli! Iacheni, ninyi watu wote mnaozungumza juu ya kuwaongoa Wayahudi. Kabla ya Ujumbe huu kumalizika, mtaona ni BWANA ASEMA HIVI, kwa Neno na kwa Roho. Israeli wataongoka wote, taifa lote, katika usiku mmoja. Biblia ilisema hivyo. Lakini Injili hata si kwa ajili yao. Kuna watoro wachache walio nje, na kadhalika namna hiyo, walioingia, na walio nje ya kundi zima la Wayahudi, walioingia na kuokolewa. Hiyo ni kweli. Ninaamini jambo hilo kwa moyo wangu—wangu wote.

Lakini, kumbukeni, mradi Israeli wako nje ya taifa lao, hawawezi kuokolewa. Sasa wanarudi. Nao wataokolewa, taifa lote, katika siku moja. Biblia ilisema hivyo. Siku moja; itawaleta, kabisa, Israeli wote wamrudie Mungu. Kutakuweko na jambo kuu mno litakaloigusa Israeli moja ya siku hizi, mpaka litalitikisa taifa zima. Hata nabii alilia kwa sauti kuu, na kusema, "Katika siku moja umefanya jambo hili." Katika siku moja, wao wataliona Hilo. Kutakuweko na jambo kuu mno.

¹²³ Kwa maoni yangu, itakuwa ni nabii mwenye nguvu atakayeinuka na kusimama mbele ya Israeli, na kuwathibitishia ya kwamba Masihi huyo angali hai. Masihi huyo waliyemkataa ni...?...

¹²⁴ Wao wakiisoma hiyo Biblia ndogo sasa, ya Biblia ya Israeli. Wao wanaisoma kinyumenyume, namna wanavyoisoma. Nanyi mnajua jinsi lugha ya Wayahudi ilivyoadikwa. Na kwa hiyo wanapoisoma... Nao wanasoma hiyo ambayo Lewi Petrus aliwatumia kule, Biblia milioni moja. Wao walisema, "Kama huyu Yesu..." Hao walikuwa ni hao Wayahudi walioletwa kutoka Iran, na kule chini, hawajawahi kusikia kitu kama Masihi. Nao walipokuwa tayari kurudi kwenye nchi ya uenyeji wao, mbona, hawangepanda kwenye ndege. Walikuwa wangali wanalima na majembe yao ya zamani. Mlisoma jambo hilo katika gazeti la *Look*. Ni wangapi waliosoma yale makala

katika gaze . . . la *Look* na la *Times*? Mbona, hakika mliyasoma. ‘Mnaona? Hawangeingia mle. Yule rabi mzee alisimama pale na kusema, “Kumbukeni, nabii wetu alisema tungerudi kwenye nchi ya uenyeji wetu kwa mbawa za tai.” Haleluya!

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
 Ishara zilizobashiriwa na Biblia;
 Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa
 na hofu;
 “Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu.”

¹²⁵ Afadhali mwamke. Mmelisikia na kulisikia jambo hilo, na kulisikia, lakini itakuwa mara ya mwisho, moja ya siku hizi. Israeli wanarudi kwenye nchi ya uenyeji wao. Siku ambayo Mungu anayakinisha Israeli kuwa taifa, hiyo ni ile siku ambayo hakutakuwepo na Mmtaifa mwингine atakayeo kolewa.

¹²⁶ Nitathibitisha jambo hilo kwa majuma haya sabini, kama tu ninaweza kuzipata siku hizo. Ninaenda kwenye . . . kutafuta kalenda za elimu ya nyota, na—na ya Julia, ile ya elimu ya nyota, na ya Kirumi, na hizo zote. Kuna nyiningine, mahali fulani. Kuna jambo fulani Mungu analijua, na, Yeye—Yeye anaweza kulifunua. Mnaona? Ninajua kalenda ya Julia ina siku mia tatu na sitini na tano na robo ya siku, katika mwaka. Kwa hiyo, loo, wao, wote wamechanganyikiwa, lakini kuna ukweli, mahali fulani.

¹²⁷ Ninaona makanisa mengi sana, madhehebu mengi sana, watu wengi sana wakienda *hivi*, na wengine, “Salamu maria,” na wengine wakiabudu *hiki*, na *kile*, *kinginecho*. Kunapaswa kuwepo na Kweli, mahali fulani. Hakuna budi kuwepo na Mungu, mahali fulani. Kunapaswa kuwepo na Ujumbe, mahali fulani. Ninawaona manabii wa uongo wakiinuka, wakiigiza upambanuzi, na kila namna ya upuuzi unaoendelea. Halafu, hakuna budi kuwe na wa kweli hapo, mahali fulani, ambamo huo wa bandia umeigizia.

¹²⁸ Ninawaona watu wakiingia katika mwili, na kupiga makelele, na kufanya yasiyofaa, na wakitoka na kuishi maisha ya kila aina. Hakuna budi kuwe na Roho Mtakatifu halisi pale, mahali fulani. Ninawaona watu wakijifanya wa kidini, na kadhalika, na kujaribu kuwa wa kidini. Ninajua kuna Mungu aliye halisi, mahali fulani. Kuna Roho halisi, mahali fulani, maana huyo ni mnafikia wa kale ambaye ameigiza, bandia wa kale. Hapana budi pawe na kitu kilicho halisi: mtu fulani, watu fulani, Kanisa fulani, Mungu fulani. Hapana budi kuwe na kitu fulani kilicho cha kweli, mahali fulani, maana hawa walinakiliwa tu kutoka kwa kitu hicho. Kuna kitu fulani ambacho ni halisi, mahali fulani.

¹²⁹ Nililiambia kanisa jambo hili, kuhusu karama zenu. [Ndugu Branham anapigapiga juu ya mimbara mara nne—Mh.] Sikilizeni karama zenu; ziwekeni katika Biblia. Msichukue

kibadala, wakati mbingu zimejaa karama za kweli. Hebu tushikilie zile zilizo halisi. Hebu na tuchukue zilizo za kweli au tusiwe na zo zote kabisa. Amina.

¹³⁰ Sasa, tukifunga, ni kweli kwamba Mungu huwashughulikia Israeli tu wanapokuwa katika nchi ya uenyeji wao. Hebu tuchukue wakati Mungu...Ibrahim alipoondoka katika nchi ya uenyeji wake akashuka akaenda huko Misri, ni jambo gani lilitukia? Yeye alitoka kwenye mapenzi ya Mungu, naye kamwe hakubarikiwa hata aliporudi kwenye nchi ya uenyeji wake. Mungu kamwe hakumshughulikia, hata ono moja, wala cho chote kile, mpaka aliporudi kwenye nchi ya uenyeji wake.

¹³¹ Waangalie Israeli wakati walipopelekwa chini huko Misri, miaka mia nne. Hakuna hata mwujiza mmoja, hakuna hata ishara moja, hakuna jambo hata moja lililotukia kati yao, halijaandikwa katika histori ya Kitabu hiki. Ni tisini na tisa ile ile ya kale: kuhudhuria kanisani, kutoa mwana-kondoo, kusema "Salamu Maria," ama cho chote kilichokuja, na kurudi. Mwaka ujao, jambo lile lile. Makuhani wote walibishana, "Rabi Fulani! Tutamchagua Rabi Fulani. Yeye ana kisomo bora zaidi. Anawajua Wamisri zaidi." Muda si muda wanajua, Wamisri na—na hao wote, walikuwa kitu kimoja.

¹³² Jambo lilo hilo ndilo limelipata kanisa. Sote tulienda kuwa Wamethodisti, ama Wabatisti, ama Wapresbiteri. "Nasi tuna digrii kutoka Hartford! Tuna digrii kutoka Wheaton! Tuna digrii kutoka mahali pengine, ama Bob Jones! Sisi, tuna Shahada ya Sanaa! Tuna D.D., LL.D., ama kitu kinginecho!" Imetufikisha wapi? Kundi la upuuzi.

Ndivyo ilivyokuwa huko Misri. Wala Mungu kamwe hajawashughulikia Israeli mpaka walipokuja kwenye nchi ya uenyeji wao.

¹³³ Nisikizeni? BWANA ASEMA HIVI, Mungu hatalishughulikia Kanisa Lake mpaka litakaporudi kwenye nchi ya uenyeji wake, Ujumbe wa wakati huu. Rudini kwenye ule wa asili! Ondokeni kwenye mawazo yenu ya Kimethodisti, Kibatisti, Kipresbiteri; yenu ya Kipentekoste, Kiasssemblies, Kiumoja, Kiutatu, na Kiutano, cho chote kile; kanisa la Mungu, Kinazarayo, Kipilgrim Holiness, kanisa la Kristo, yote ni mashirika ya upinga-Kristo! Nami ninatambua ya kwamba huu unasambazwaa ulimwenguni. Yote yako makosani; yote ni ya Ibilisi. Loo, jamani! Kuna wacha Mungu katika kila moja la hayo. Kuna wacha Mungu katika kila moja ya mashirika hayo. Lakini hilo shirika, lenyewe, si la Mungu, na kamwe Mungu hatalibariki. Yeye kamwe hajayabariki.

¹³⁴ Ninamwuliza mwanahistoria ye yote (mtakaoisikia kanda hii) kunindikia na kuniambia wakati wo wote, kanisa lilipouna madhehebu, kama Mungu hakuliweka kwenye rafu wala hakulishughulikia tena. Niambie ni wakati gani Yeye

alipowainua Waluteri tena, Wesley na Wamethodisti, ama Mpentekoste. Kamwe hajawainua! Madhehebu hayo yalikaa pale, yakaoza na kuharibika! Mungu aliwachukua watu binafsi na kujaribu kuwaelekeza watu warudi kwenye nchi ya uenyeji wao. Halafu basi, hao watu binafsi wakawa wanyonge sana na dondoadume, wakiwa na namna fulani ya digrii, mpaka wakaunda madhehebu mengine, wakayafanya mtoto maradufu wa kuzimu zaidi kuliko yalivyo kuwa hapo mwanzoni.

¹³⁵ Lakini, mahali fulani, hakika, Yehova ana mtu ambaye anaweza kumwekea mikono Yake, ambaye hatapatana nao... . . . yamchayo, madhehebu yasiyomcha Mungu; ambaye atawatikisa watu kuwarudisha kwenye ule Mwamba, Kristo Yesu, kuwarudisha kwenye pentekoste ya awali na Roho Mtakatifu wa awali, yenyе ishara na maajabu ya asili. Hakika ana mmoja, mahali fulani, ambaye hatavunjika chini ya namna yo yote ya mateso, atoroke, afutilie mbali, aanguke, wala cho chote kile; ambaye atadumu nalo.

Mungu kamwe hawabariki Israeli mpaka wamerudi kwenye nchi ya uenyeji wao.

¹³⁶ Mungu hatakubariki kamwe, Mmethodisti, Mbatisti, Mpresbiteri, Mkatoliki, wala Mpilgrim Holiness, Mnazarayo, kanisa la Kristo, ama—ama madhehebu ya Kipentekoste. Hatakubariki hivyo mlivy. Rudini kwenye nchi ya uenyeji wenu, mwanzoni, rudini kwenye tukio la kipentekoste kama lilivyo tukia kwenye Siku ya Pentekoste wakati Nguvu za Mungu aliye hai zilipobadilisha hao maelfu ya watu, na kuuwasha moyo wao kwa Moto wa Mungu, ulionyesha zile za kweli; si ishara zilizoigwa, si kushirikishana mawazo kwa bandia, si igizo fulani, na kuingia katika mashindano ya kufa na kupona kama tuliyoo nayo hapa Marekani. “Ni nani anayeweza kupata hema iliyo kubwa kuliko zote?” Ama, “Ni nani anayeweza kuwa na kundi kubwa kuliko wote?” Inaleta tofauti gani kwa Mungu? Mungu anawataka watu walio waaminifu moyoni, si umati mkubwa wa watu. Nasi sote tuna shindano la kufa na kupona hapa, tunakimbia mbio. Ni fedheha iliyoje, kuona kama tunaweza kuongezea elfu moja zaidi kwenye madhehebu yetu. Ni fedheha. Yeye anatutaka turudie ile Kweli, turudi kwake Roho, turudi kwenye Nuru ya kweli, turudi kwenye njia kuu katika Kristo, turudi kwenye ile Kweli. Anawezaje kamwe kutubariki kwa jinsi tunavyofanya? Hatatubariki.

¹³⁷ Yeye kamwe hakuwabarikia Israeli mpaka waliporudi kwenye nchi ya ahadi. Na hapo waliporudi kwenye nchi ya ahadi, ishara na maajabu yalianza kutukia. Yeye alimtuma mtu moja kwa moja mionganii mwao, jina lake Musa. Musa huyu alishuka na kitu gani, theolojia iliypigwa msasa? Je! yeye alikuja na Shahada ya Sanaa? Je! yeye alishuka na LL.D., Ph.D.? Yeye alishuka na nguvu za Yehova, na ujumbe, “Rudini, kutoka

kwenye nchi hii, mwende katika nchi ya uenyeji wenu. Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu.” Amina!

¹³⁸ Kwa karibu miaka elfu mbili, Wayahudi wamekuwa nje ya nchi ya uenyeji wao, wametawanywa katika pepo nne za dunia. Jinsi ambavyo tungeweza kuufanya Ujumbe huu uendelee kwa majuma kadha sasa, kama tungeingia kwenye kilindi chake. Tunaweza kuwafuatilia Israeli moja kwa moja huko nyuma na kuonyesha wakati walipotawanywa na Himaya ya Kirumi, baada ya kumkataa Masihi; jinsi walivyofukuzwa wakaenda katika kila taifa chini ya Mbingu.

Turudi kwa Yakobo, Israeli, turudi katika Mwanzo 44 na 45, na kuonyesha huko nyuma vile alivyowabariki hao wazee na kuwaambia mahali pao watakapokuwa hasa katika siku za mwisho. Nami ninaweza kuwaonyesha kabisa (kila taifa) la Israeli, kila kabilia la Israeli, likisimama kabisa katika mataifa ambapo ilisema watakuwa. Na sasa tumewasili.

¹³⁹ Myahudi ambaye tunamjua, huyo si Myahudi halisi hasa. Myahudi halisi ni yule Mworthodoksi ambaye hajajichafua na mambo ya ulimwengu, ambaye hajatoka nje na kujiunga na makanisa mengine. Hao ndio wanaorudi huko ng’ambo, waishio kwa jibini na mkate, huko kwenye mimba ya vilima, wasiokubaliwa katika ule mji wa kale. Iliwabidi kujenga mji upande huu, katika nchi isiyo ya mtu, ambapo bom bom zimeelekezwa pande zote mbili. Lakini ameanza kuchipuza matawi yake. Amina, na amina! Wakati umekaribia.

¹⁴⁰ Hao hapo Ishmaeli na Isaka, wamesimama pale, wakibishania juu ya nchi hiyo, bado, lakini ni ya Israeli. Ikitokea kwamba uende katika Yerusalemu mpya, hawatakuruhusu kuingia katika Yerusalemu ya kale. Itakubidi kwenda kule kwanza na kuwaacha wakuelezee yote, hao Waarabu, ndipo wakupeleke upande huo mwingine. Hao ni watoto wa Ishmaeli. Lakini, ngoja, utakuja wakati ambapo watoto wa Mungu wataiteka. Hiyo ni kweli. Yerusalemu itajengwa upya tena. Sadaka ya kila siku itaanzishwa.

Na mpinga-Kristo atafanya agano kwa hayo majuma saba ya mwisho. Na katikati ya hayo, atavunja agano hilo, awaingize wote kwenye Ukatoliki. Chukizo litaenea juu ya mahali pote, namna hiyo, na hapo ndipo ule mwisho utakapokuja.

¹⁴¹ Angalia, “majuma sabini.” Naam, wana karibu miaka elfu mbili nje ya nchi yao. Sasa wamefukuzwa. Wao ni watu kama ilivyokuwa katika kule kuufanya mgumu moyo wa Farao. Ilimbidi kuufanya mgumu moyo wa Hitler. Mamilioni yao walikuufa. Mwangalie huyu Eichmann, mwenye hatia ya kuwaua Wayahudi milioni sita. Watu milioni sita, nafsi za wanadamu, watoto wachanga, watoto, watu wazima, wote waliuawa; Eichmann, mtu mmoja. Angalia Urusi, jinsi ilivyowafukuza

kutoka kule. Waliwafukuzwa kila mahali. Wamekuwa taifa lililodharauliwa.

¹⁴² Lakini kwa sababu ya kupenda fedha kwao, walirudi tena. Lakini kundi hilo dogo linalarudi kule Palestina. Amina, ndugu! Utakapowaona wakianza kurudi kwenye nchi ya uenyeji wao!

¹⁴³ Sasa wana watu wa kutosha kule kufanya hiyo kukaribia mia na arobaini na nne elfu. Na ni jambo gani linalotukia? Wao watamjua Yusufu wao. Msijali. Naam, bwana. Nao wote wanasmama kule wakingojea jambo hilo litukie. Na ile saa ambayo hasa...

¹⁴⁴ Mataifa yamewatangaza kwamba wao ni taifa, mwaka huu uliopita. Jambo hilo litakapotendeka, tuko karibu na mwisho, Kanisa la Mataifa limeondoka. Kwa hiyo, karibu wakati wo wote, Mungu angeweza kusema, “Israeli ni watu Wangu.” Hilo litakapotukia, Mataifa wamekwisha.

¹⁴⁵ “Watakanyaga,” kasema Yesu, katika Mathayo 24. “Chukizo la uharibifu, watakanyaga kuta za Yerusalemu hata wakati wa Mataifa utakapotimia.” Wakati hayo yatakapokwisha, ndipo Wayahudi watakaporudi Yerusalemu, kuanzisha upya lile hekalu na ibada za hekaluni. Tutapata jambo hilo lote katika Jumbe hizi zinazokuja, majuma sabini ya zile sababu sita.

Sasa nitazisoma hizo kabla sijafunga, maana karibu saa imewadnia kwa sisi kwenda nyumbani, halafu turudi usiku kwenye saa moja.

¹⁴⁶ Kwanza, kwanza, kama unaliandika, “Ili kukomesha makosa.” Danieli, sura ya 9, aya ya 24. “Kukomesha makosa,” moja. “Kuishiliza dhambi,” mbili. “Kufanya upatanisho kwa ajili ya uovu,” tatu. “Kuleta haki ya milele,” nne. “Kutia muhuri ono na unabii,” tano.” “Kumtia mafuta ye ye aliye Mtakatifu sana,” sita. Na hilo ndilo ambalo tutazungumzia usiku wa leo. Mungu, akitimiza!

¹⁴⁷ Sasa ngoja, hebu nilirudie tena, ili mlipate. Kwanza, “kukomesha makosa.” Pili, “kuishiliza dhambi.” Tatu, “kufanya upatanisho kwa ajili ya uovu.” Nne, “kuleta haki ya milele.” Tano, “kutia muhuri ono na unabii.” Sita, “kumtia mafuta aliye Mtakatifu sana.”

Hebu niwasomee hilo sasa, kutoka—kutoka kwenye Biblia. Ni aya ya 24.

Sabin...majuma sabini umeamriwa juu ya watu wako, (Wayahudi) na juu ya mji—juu ya mji wako mtakatifu, (Israeli, Wayahudi, Yerusalemu), ili kukomesha...makosa (moja),... kuishiliza dhambi (mbili),...kufanya upatanisho kwa ajili ya uovu (tatu),...kuleta haki ya milele (nne), na kutia muhuri maono (tano)—ono na unabii, na kumtia mafuta ye ye aliye Mtakatifu sana (sita).

¹⁴⁸ Hayo ndiyo hasa Yeye aliyokuja kumwambia, yatakayotendeka, ndipo mwisho uje.

¹⁴⁹ Sasa, usiku wa leo tutaona mambo hayo ni nini, na tuone jinsi tulivyo karibu na mahali hapo. Ndiposa Jumapili ijayo, tutaingiza na kuweka kwenye mahali pake mambo haya ya wakati mahali pale hasa tunaposimama. Ninampenda.

¹⁵⁰ Israeli wanarudi katika nchi ya uenyeji wao, huko Israeli. Hebu niseme tu jambo hili wakati... Nadhani kinasasauti kimefungwa. Hebu niseme jambo hili. Saa ile ile ambayo Israeli walifanyika taifa... Sababu ambayo nimeamini daima, mbele ya darasa langu hapa, ya kwamba kulikuwa na jambo fulani ningeshiriki, kabla sijafa, la kuwarudisha Israeli kwa Bwana. Kwa sababu, wakati saa ile ile, kwa jedwali la Pan Amerikan, ambapo Israeli walitangazwa kuwa taifa, kwa mara ya kwanza katika miaka elfu mbili tangu watawanywe, si taifa tena; ilikuwa ndiyo saa ile ile hasa, ambapo Malaika wa Bwana alikutana nami kule na kunituma kwa... na Injili. Jambo lile lile, tarehe 7 Mei, 1946.

¹⁵¹ Sasa, basi, jambo lingine linalonifanya kujua. Ni “kugeuza mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, na mioyo ya baba iwaelekee watoto wao,” ule Ujumbe. Angalia, Malaki 4 (si 3), 4!

¹⁵² Jambo lingine. Wakati, Billy, mimi na mwanangu, Ndugu Ern Baxter, tulipokuwa tukienda zetu Palestina, baada ya kukutana na Wayahudi kwa Ndugu Arganbright, nao wakauona huo m kutano. Lewi Pethrus alikuwa ametuma Biblia hizi kule. Naye akasema... Wayahudi hawa walikuja, wakasema, “Kama utaita kundi la viongozi wa Israeli, ninamaanisha, si hawa marabi wa kisasa na sherehe zao zote, lakini uwakusanye viongozi weneyewe hasa wa Israeli pamoja. Nasi tumesoma Agano hili Jipy, na tunajua ya kwamba Masihi atakapokuja, Yeye atatwambia mambo haya, kama yule mwanamke kule Samaria. Tunajua ya kwamba Musa alisema Masihi wetu atakuwa nabii. Na utakapoweza kuwaambia na kuwaonyesha, kwa Maandiko,” jambo hilo ambalo tutapata katika Ujumbe wa usiku wa leo, “ya kwamba iliwabidi kutiwa giza na mioyo yao kukatwa, ili kwamba nafasi ya Mataifa ije, ili kwamba tuwe na wakati wa kupatanishwa kwa Mataifa. Nayo mioyo yao ilifanywa migumu kama vile vile ilivyokuwa katika wakati wa Yusufu, na kadhalika. Na ndipo tuwalete hao Wayahudi mpaka mahali fulani, na kuwaita watu hao kutoka mionganoni mwa watu waliopo, kama tu vile unavyowafanya hawa Mataifa hapa, kwa uvuvio huo wa Roho.” Maana, wao walisema, “Kama Yesu huyu, kama Yeye ndiye Masihi, na maneno yako ni kweli, basi Yeye si mfu, pia yu hai. Na kama Yeye yu hai, Yeye aliahidi kuwa katika ninii Yake... mtu-... mtumishi Wake—watumishi, wanafunzi Wake. Basi kama tunaweza kumwona akifanya ishara ya nabii, basi tutaamini ya kwamba Yeye ni Masihi.”

Ni jambo kamilifu namna gani, kweli kabisa. Basi, jambo hilo lingefanya nini? Taifa lingezaliwa katika siku moja, mionganoni mwa viongozi. Kila mmoja wao angesema, "Tunajua jambo hilo." Huyo rabi anaposema jambo hilo, hilo linatosha. Taifa litazaliwa katika siku moja. Israeli ingezaliwa katika siku moja.

¹⁵³ Nami nilikuwa nikienda zangu, ndipo nikasimama Cairo, Misri, tikiti ikiwa mkononi mwangu, na zimesalia dakika kumi na tano tuitwe. Wao walikuwa wakijiandaa kutangaza. Ndipo nikashuka nikaenda kuangalia kipande cha huu mpingo, kilichokuwa kimechongwa sanamu ya ndovu mdogo kwa mpingo, akiwa na pe—pembe za kipusa. Nilikuwa niitumie rafiki yangu daktari, Dr. Sam Adair, kama ya kukandamizia karatasi. Nami nilikuwa nikiiangalia. Ndipo kitu fulani kikaniambia, "Wakati haujawadia bado. Iache Palestina."

¹⁵⁴ Kwa hiyo nikawaza, "Hiyo ilikuwa ni mimi tu nikiwazia jambo hilo." Ndipo nikaendelea.

Kitu Fulani kikasema, "Huu sio wakati wake."

¹⁵⁵ Ndipo nikatoka nikaenda nyuma ya lile banda. Nikainua kichwa changu kwa Mungu. Nikasema, "Mungu, je! ni Wewe uliyekuwa ukinena nami?"

¹⁵⁶ Kasema, "Wakati haujawadia. Usiende Palestina. Wakati haujatimia." Ndipo nikachukua tikiti yangu na kuibadilisha, nikatoka huko nikaenda kupitia Rumi, ndipo nikarudi Lisbon, katika Ureno, halafu kutoka kule nikarudi Marekani.

¹⁵⁷ Saa ilikuwa haijawadia bado. Maovu ya Mataifa hayajaja bado, mpaka pomoni mwa kikombe. Lakini siku moja hilo litatimia, ndipo Mungu atamtuma mtu fulani kule ambaye ni nabii, naye atawathibitishia. Ninatumaini ya kwamba Mungu atamwinua mara moja, ye yote yule, ambaye atamwinua upesi. Ninaamini jambo hilo halina budi kuja. Hiyo ndiyo sababu ya sisi kujifunza hili, kwamba tumekaribia sana.

¹⁵⁸ Na, kumbukeni, dakika ile ile ambapo Wayahudi watampokea Kristo, Kanisa la Mataifa limeondoka. Ndipo Mataifa watamwagiwa mapigo, ile Dhiki.

¹⁵⁹ Basi—basi watu, waalimu mashuhuri wanawezaje kufundisha, na huku wanaingalia Biblia hii namna hii, na kusema ya kwamba Kanisa litapitia kwenye ule wakati wa ile Dhiki, wakati hakuna Maandiko katika Biblia yanayosema jambo hilo! Hawana jambo hata moja.

¹⁶⁰ Mtu fulani aliniambia, si muda mrefu uliopita, kasema, "Loo, Dada McPherson alifundisha ya kwamba Kanisa lingepitia kwenye ile Dhiki, maana tutakuwa mianga ing'aayo katika wakati huo." Ni Israeli wakati huo, si Mataifa.

Mataifa tayari wameondoka, lile Kanisa. Haitawabidi kupitia katika Dhiki yo yote. "Lile joka lilitapika maji kutoka

katika kinywa chake,” sura ya 17, “na kufanya vita na wale masalia,” yule mwanawali mjinga. Si...lile kanisa halisi liliondoka. Yeye yuko kwenye Karamu ya Arusi kwenye ninii hizi, kipindi cha wakati ambapo Karamu ya Arusi itakuwa inaendelea, lile juma la mwisho. Na hapo ndipo ile Dhiki itakapoanza, wakati wale nzige na mateso yatakapoinuka juu ya makanisa, mambo kama hayo.

Kisha, mwishoni, katika sura ya 19, Huyu hapa anakuja pamoja na Bwana Arusi Wake. Haleluya! “Mfalme wa wafalme, na Bwana wa mabwana; vazi lililochovywa katika Damu, na majeshi ya Mbinguni yamepanda farasi weupe, wakija pamoja Naye. Huyo hapo Bibi-arusi anakuja, kuchukua mahali Pake kwa ajili ya ule Utawala wa Miaka Elfu. Amina! Loo!

Heri ni Jina, loo, heri ni Jina,
Heri ni Jina la Yesu;
Heri ni Jina, loo, heri ni Jina,
Heri ni Jina la Yesu.

Yesu ni Jina, Yesu ni Jina,
Yesu ni Jina la Bwana;
Yesu ni Jina, Yesu ni Jina,
Yesu ni Jina la Bwana.

Tukuza Jina, loo, Tukuza Jina,
Loo, tukuza Jina, loo, la Bwana;
Tukuza Jina, loo, Tukuza Jina,
Loo, tukuza Jina la Bwana.

¹⁶¹ Unalitukuza namna gani? Unalitukuza katika maisha yako. Unaishi maisha mazuri hivi kwamba wao wanaweza kusema, “Huyo hapo mtumishi wa Kristo.” Hivyo ndivyo unavyolitukuza Jina hilo. Hebu tuone. Loo, je! Hamumpendi? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Loo, jamani! Wimbo wetu mdogo sasa:

Katika hori zamani za kale, ninajua ndivyo
ilivyo kweli,
Mtoto mchanga alizaliwa awaokoe watu
kutoka katika dhambi yao.
Yohana alimwona ufukoni, Mwana-Kondoo
wa milele,

Huyo Mwana-Kondoo mwenye hiyo Mihuri saba, Ndiye tu pekee Mbinguni na nchini aliyeweza kukitwaa. Katika hor-...

Katika hori zamani za kale, ninajua ndivyo
ilivyo kweli,
Mtoto mchanga alizaliwa awaokoe watu
kutoka katika dhambi yao.
Yohana alimwona ufukoni, Mwana-Kondoo
wa milele,
Loo, heri ni Jina.

Loo, heri ni Jina, loo, heri ni Jina,
 Heri ni Jina la Yesu;
 Heri ni Jina heri ni Jina,
 Heri ni Jina la Yesu.

¹⁶² Ninapenda kuabudu. Nanyi je? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa, hatuji kanisani kusikia tu mahubiri; hayo yanaambatana nalo. Lakini tunakuja kanisa kuabudu, kuabudu katika Roho na Kweli. Mmesikia Kweli; hilo ni Neno. Unaona? Sasa, kuabudu, ni kujieleza Kwake. Mnaona?

Loo, Nampenda Yule Mtu wa Galilaya! Tupe sauti kidogo ya huo. Naam, bwana. Unauju, Teddy? Ninasahau sasa. Hebu tuone. Hebu tuone.

Loo, nampenda yule Mtu wa Galilaya, wa Galilaya,

Kwa kuwa Yeye amenitendea mengi.

Amenisamehe dhambi zangu zote, akaweka Roho Mtakatifu ndani yangu;

Loo, nampenda, nampenda yule Mtu wa Galilaya.

Mtoza ushuru alienda kuomba kule hekaluni siku moja,

Akalia, “Ee Bwana, unirehemu!”

Alisamehewa kila dhambi, na amani kuu ikawekwa ndani yake;

Akasema, “Njoni, mumwone huyu Mtu wa Galilaya.”

Loo, nampenda yule Mtu wa Galilaya, wa Galilaya,

Kwa kuwa Yeye amenitendea mengi.

Amenisamehe dhambi yangu yote, akaweka Roho Mtakatifu ndani yangu;

Loo, nampenda, nampenda yule Mtu wa Galilaya.

Viwete walifanywa watembee, bubu walifanywa wanene.

Nguvu hizo zilinenwa kwa upendo juu ya bahari.

Vipofu walifumbuliwa macho, ninajua ingaliweza kuwa tu

Ni kwa nguvu za huyo Mtu wa Galilaya.

Loo, nampenda yule Mtu wa Galilaya, wa Galilaya,

Kwa kuwa Yeye amenitendea mengi.

Amenisamehe dhambi zangu zote, akaweka Roho Mtakatifu ndani yangu;

Loo, nampenda, nampenda yule Mtu wa Galilaya.

Usikilizeni huu.

Yule mwanamke kisimani, Yeye alimwambia
dhambi zake zote,
Jinsi alivyokuwa na wanaume watano wakati
huo. (Huyo Ndiye.)
Alisamehewa kila dhambi, ndipo amani kuu
ikaingia ndani yake;
Ndipo akasema, "Njoni, mumwone yule Mtu
wa Galilaya!"

Loo, nampenda yule Mtu wa Galilaya, wa
Galilaya,
Kwa kuwa Yeye amenitendea mengi.
Amenisamehe dhambi zangu zote, akaweka
Roho Mtakatifu ndani yangu;
Loo, nampenda, nampenda yule Mtu wa
Galilaya.

Ninampenda. Nanyi je? [Kusanyiko linasema, "Amina."—
Mh.] Moyo wangu wote! Nanyi je? ["Amina."] Yeye si ni wa
ajabu? ["Amina."]

Loo, wajabu, wajabu, Yesu ni wangu, (Yeye ni
nini?)
Mshauri, Mfalme, Yeye ni Mungu;
Loo, huniokoa, hunilinda na dhambi na aibu,
Waajabu ni Mkombozi, asifiwe!

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa na tuwazie jambo hilo.

Siku moja nilikuwa nimepotea, lakini sasa
nimepatikana, niko huru na hukumu,
(mataifa yanavunjika; haidhuru)
Yesu hunipa uhuru na wokovu kamili;
Huniokoa, hunilinda na dhambi na aibu,
Wajabu ni Mwokozi, asifiwe.

Loo, wajabu, wajabu, Yesu ni wangu,
Mshauri, Mfalme, Yeye ni Mungu;
Loo, huniokoa, hunilinda na dhambi na aibu,
Waajabu ni Mkombozi, asifiwe!

Loo, wazia jambo hilo!

Siku moja nilikuwa nimepotea, sasa
nimepatikana, niko huru na hukumu,
Yesu hunipa uhuru na wokovu kamili;
Huniokoa, (Yeye hufanya kitu gani?) hunilinda
na dhambi zote na aibu, (ninapaa juu yake)
Loo, waajabu ni Mwokozi, asifiwe.

Sasa sote pamoja!

Loo, wajabu, wajabu, Yesu ni wangu,
 Mshauri, Mfalme, Yeye ni Mungu;
 Mbona, huniokoa, hunilinda na dhambi na
 aibu,
 Waajabu ni Mkombozi, asifiwe!
 Loo, Yesu nakupenda,
 Loo, Yesu nakupenda . . .

Nina furaha sana kwamba nimeokolewa! Nina furaha sana
 kwamba ninakungojea Kuja Kwake!

Loo, Yesu nakupenda, (utukufu!)
 Kwani alinipenda kwanza.

Sasa huku tumeinua mikono yetu juu, kama tunamaanisha
 jambo hilo.

Loo, mimi sitamwacha,
 Loo, mimi sitamwacha,
 Loo, mimi sitamwacha,
 Kwani alinipenda kwanza.

¹⁶³ Mnampenda? [Kusanyiko linasema, “Naam.”—Mh.] Basi
 hamna budi kupendana. Maana, kama huwapendi wale
 unaoweza kuwaona hata hapa, unawezaje kumpenda Yeye
 Ambaye hujapata kumwona? Na tupeane mikono sisi kwa sisi,
 tuseme:

Loo, Yesu nakupenda,
 Loo, Yesu nakupenda,
 Loo, Yesu nakupenda,
 Kwani ulinipenda kwanza.

Loo, mimi sitamwacha,
 Mimi sitamwacha,
 Mimi sitamwacha,
 Kwani alinipenda kwanza.

¹⁶⁴ Wazia tu, Yeye alitufahamisha huo ufunuo mkuu. Si
 tunampenda? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Yeye si ni
 wa ajabu? [“Amina.”] Jinsi tulivyo na shukrani kwa ajili ya
 Bwana wetu Yesu; hajapata kutuacha. “Loo, niko pamoja nanyi
 siku zote, hata . . .” Je! mnayafurahia *Majuma Sabini Ya Danieli?*
 [“Amina.”] Loo, si tunampenda? Yeye anafanya jambo hilo
 namna gani?

Yesu kwa imani,
 Nakutumaini,
 Peke Yako . . .

Mwabuduni tu, kutoka moyoni mwako.

Nikisie sasa,
 Na kunitakasa
 Ni Wako kabisa
 Tangu leo!

Hapa nazunguka, (sote huzunguka)
 Katika mashaka, (Naam, Bwana)
 Na matata,
 Palipoo na giza, utaniongoza (Niongoze
 kupitia gizani, Bwana.)
 Utaniongoza,
 Hivi nitaweza
 Kufuata.

[Ndugu Branham anaaza kuvumisha *Yesu Kwa Imani*]
 Za kusaidia
 Moyo wangu;
 Ulikufa Wewe,
 Wokovu nipewe,
 Nakupenda Wewe
 Bwama Wang!

¹⁶⁵ Loo Yesu, tunaona tunakaribia jambo fulani. Nabii Isaya alikuwa amenena habari zake; Yeremia alikuwa amenena habari zake. Danieli aliangalia nyuma akaona walioyokuwa wamesema. Iliufanya moyo wake kuchangamka, naye—naye akauelekeza uso Wake Mbinguni. Akafunga, nguo za magunia na majivu. Alitaka kusikia, ili kwamba aweze kuwaonya watu.

¹⁶⁶ Bwana, tunaona kwa Vitabu, pia, Kitabu Chako, Kitabu cha Isaya, Kitabu cha Yeremia, Kitabu cha Yakobo, Yohana, Luka, Marko, Mathayo, Kitabu cha Ufunuo, Vitabu Vyako vyote, ya kwamba tuko karibu na mwisho. Nasi tumezielekeza nyuso zetu Mbinguni, katika maombi, kusihi, kuona mahali tunapoishi, Bwana. Tunaanza kuona siku ikipambazuka. Na, Bwana, tunakuja Kwako. Imani Yetu imeelekezwa Kwako sasa. Tukiweka kando kila mzigo, na kila dhambi, kila kutokuamini kudogo ambako kungetizinga kwa upesi, tunakaza mwendo sasa kuelekea mede ya wito mkuu, tukijua ya kwamba wakati wetu ni mdogo.

¹⁶⁷ Wabariki watu hawa hapa ndani, Bwana. Wao wanakupenda. Wao ni wako. Wametoka. Wewe ndiwe unayefunua. Tunaomba ya kwamba utatujalia mambo haya tunapokungojea.

¹⁶⁸ Tupe alasiri njema ya kusoma, Bwana. Tupe ufahamu. Turudishe tena usiku wa leo, wenye nguvu. Bwana, nitie upako lasiri hii, ee, Bwana, ninaposoma zile sababu sita za kuzuru kwa Gabrieli. Kama Gabrieli alikuja kuzuru na akatoa maana sita, Bwana, hatuna budi kujua hayo. Tumesovisoma vitabu na kujua ya kamba tuko karibu. Kwa hiyo tunaomba ya kwamba Wewe utatufunulia sisi usiku wa leo.

¹⁶⁹ Jumapili ijayo, Bwana, Ee Mungu, ziingize hizo siku humo. Sijui, lakinii Wewe unaweza kutuleta moja kwa moja kwenye wakati huo. Tujalie hilo, Baba. Tunakutumainia Wewe.

Tunapendana sisi kwa sisi na Damu ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, imetusafisha na dhambi zote. Tunakuangalia Wewe sasa. Tusaidie tunapokungojea Wewe, Baba, katika Yesu Bwana wetu.



Maagizo Ya Gabrieli Kwa Danieli
(Gabriel's Instructions To Daniel)
30 Julai, 1961, Jumapili asubuhi

Sababu Sita Za Kusudi La Gabrieli Kumzuru Danieli
(The Sixfold Purpose Of Gabriel's Visit To Daniel)
30 Julai, 1961, Jumapili jioni

Lile Juma La Sabini La Danieli
(The Seventieth Week Of Daniel)
6 Agosti, 1961, Jumapili asubuhi

Jumbe hizi za Ndugu William Marrion Branham zilihubiriwa kwenye Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani. Baada ya kupata kanda za awali ambazo zinasikika vizuri na ni kamili zaidi, kitabu hiki cha Neno Lililonenwa cha *Yale Majuma Sabini Ya Danieli* kimechapishwa tena kwa mpangilio wa sasa. Kila jithada imefanywa kuhamisha kwa usahihi Ujumbe wa sauti kutoka kwenye kanda za sumaku zilizorekodiwa na kuuandika katika kitabu, na umechapishwa hapa bila kufupishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Uilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2001 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org